Ilani ya Kuhifadhi Utaratibu

Sehemu B ya Sheria ya Elimu ya Watu Walemavu (IDEA).

Kumbuka: Marejeo yote ya wilaya ya shule yanatumika kwa chombo cha umma kinachowajibika.

Faharasa

Habari kwa Ujumla 1
Ilani Iliyoandikwa Mapema 1
Lugha Asili 2
Barua ya Elektroniki 2
Ruhusa ya Mzazi - Ufafanuzi 2
Ruhusa ya Mzazi 3
Tathmini zenye Kujitegema za Kielimu 5

Usiri wa Habari 7
Ufafanuzi 7
Inayoweza Kutambuliwa na Mtu Binafsi 7
Ilani kwa WAzazi 7
Haki za Ufikiaji 8
Rekodi ya Ufikiaji 8
Rekodi za Zaidi ya Mtoto Mmoja 9
Orodha ya Aina na Maeneo ya Habari 9
Ada 9
Kurekebishwa kwa Rekodi Mzazi Akiomba 9
Nafasi ya Kusikilizwa 9
Utaratibu wa Kusikilizwa 10
Matokeo ya Kusikilizwa 10
Ruhusa ya Kufichua Habari za Kibinafsi zinazoweza Kutambuliwa 10
Kuhifadhi 11
Uharibifu wa Habari 11

Utaratibu wa Malalamiko ya Serikali 11
Utofauti kati ya Malalamiko ya Kusikilizwa kwa Mchakato Unaotazamiwa na Utaratibu wa Malalamiko ya Serikali 11
Kuchukuliwa kwa Utaratibu wa Malalamiko ya Serikali 12
Utaratibu wa Chini wa Malalamiko ya Serikali 12
Kuwasilisha Malalamiko ya taifa 13

Harakati ya Utaratibu wa Malalamiko Unaotazamiwa 14
Kuwasilisha Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa 14

Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa *15*
Fomu za Mfano *16*
Upatanisho *17*
Mchakato wa Suluhisho *18*

Harakati ya Kusikilizwa Kwa Malalamishi Inayotazamiwa **20**
Kusikilizwa kwa Mchakato adilifu unaotazamiwa *20*
Haki za Kusikilizwa *21*
Maamuzi ya Kusikilizwa *22*

Rufaa **23**
Kukamilika kwa uamuzi; Kukata rufaa; Uhakiki adilifu *23*
muda maalum na Urahisi wa Kusikilizwa na Uhakiki *23*
Hatua za Madai, Pamoja na Kipindi cha Muda ambao Unaweza Kuwasilisha Hatua hizo *24*
kuwekwa kwa mtoto wakati wa mCHAKATO UNAOTAZAMIWA malalamishi na kusikizwa kwa kesi kukiwa bado kunagojewa *25*
Ada ya Wakili *25*

Utaratibu Unaofuatwa Wakati wa Kuadhibu Watoto Wenye Ulemavu **27**
mamlaka ya mtumishi wa shule *27*
Mabadiliko ya Mahali kwa Sababu ya Uhamisho wa Kinidhamu *30*
Uamuzi wa Mpangilio *30*
Kukata rufaa *30*
Mahali Wakati wa Kukata rufaa *32*
Ulinzi kwa Watoto ambao Hawajastahiki Elimu Maalum na Huduma Zinazolingana *32*
Rejeleo la hatua ya Watekeleza Sheria na Watawala wa kimahakama *33*

Matakwa ya Mahali pa Taifa moja ya Wazazi wa Watoto walio katika Shule za Kibinafsi kwa Gharama ya Umma **33**
Kwa ujumla *33*

HABARI KWA UJUMLA

ILANI ILIYOANDIKWA MAPEMA

34 CFR §300.503

Ilani

Wilaya ya shule yako ni lazima ikupe ilani iliyoandikwa (ikupe habari maalum kwa kuandika), kati ya wakati mwafaka kabla ya:

1. Pendekeza kuanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini, au mahali pa elimu ya mtoto wako, au utoaji wa elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) kwa mtoto wako;

   au

2. Kataa kuanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini, au mahali pa elimu ya mtoto wako, au utoaji wa FAPE kwa mtoto wako.

Yaliyomo kwenye ilani

Ilani iliyoandikwa ni lazima:

1. Ifafanue hatua ambayo wilaya ya shule yako inapendekeza au inayokataa kuchukua;
2. Ieleze ni kwanini wilaya ya shule yako inapendekeza au inakataa kuchukua hatua hiyo;
3. Ifafanue kila utaratibu wa tathmini, uchunguzi, rekodi, au ripoti ambayo wilaya ya shule yako ilitumia katika kuamua kupendekeza au kukataa hatua hiyo;
4. Ijumuishe taarifa ya kwamba una ulinzi chini ya utoaji wa kuhifadhi utaratibu katika Sehemu B ya IDEA;
5. Ikuambie vile unavyoweza kupata ufafanuzi wa kuhifadhi utaratibu kama hatua ambayo wilaya ya shule yako inapendekeza au inakataa sio rejeleo halisi la tathmini;
6. Ijumuishe rasilimali unazoweza kurejelea ili kukusaidia kuelewa Sehemu B ya IDEA;
7. Ifafanue chaguzi zingine ambazo Kikundi cha mpango wa elimu ya kibinafsi ya mtoto wako (IEP) ilionelea na sababu ambazo chaguzi hizo zilikataliwa; **na**
8. Itoe ufafanuzi wa sababu zingine za kwanini wilaya ya shule yako ilipendekeza au ilikataa hatua hiyo.

Ilani katika lugha inayoeleweka

Ilani lazima iwe:

1. Imeandikwa katika lugha inayoeleweka na umma kwa ujumla; **na**
2. Imetolewa katika lugha yako ya asili au hali nyingine ya kuwasiliana unayotumia, isipokuwa kama haiwezi kufanyika hivyo waziwazi.

Ikiwa lugha yako ya asili au hali nyingine ya kuwasiliana sio lugha iliyoandikwa, wilaya ya shule yako ni lazima ihakikishe kwamba:

1. Ilani hiyo imetafsiriwa kwa kusema au kwa hali zingine katika lugha yako ya asili au hali nyingine ya kuwasiliana;

2. Unaelewa yaliyomo kwenye ilani; **na**
3. Kuna ushahidi ulioandikwa ya kwamba 1 na 2 walipatana.

LUGHA ASILI

34 CFR §300.29

Lugha asili, inapotumiwa na mtu ambaye afahamu Kiingereza vizuri, inamaanisha yanayofuata:

1. Lugha ambayo kwa kawaida inatumiwa na mtu huyo, au, kwa hali ya mtoto, lugha ambayo kwa kawaida hutumiwa na wazazi wa mtoto;
2. Katika kuwasiliana moja kwa moja na mtoto (ikijumuisha tathmini ya mtoto), lugha ambayo kwa kawaida hutumiwa na mtoto nyumbani au katika mazingira ya kujifunza.

Kwa mtu ambaye ni kiziwi au kipofu, au mtu ambaye hana lugha iliyoandikwa, hali ya mawasiliano ni ile mtu huyo kwa kawaida hutumia (kama vile lugha ya ishara, au mawasiliano ya kusema).

BARUA YA ELEKTRONIKI

34 CFR §300.505

Ikiwa wilaya ya shule yako inawapa wazazi chaguo la kupokea hati kwa barua pepe, unaweza kuchagua kupokea yafuatayo kwa barua pepe:

1. Ilani iliyoandikwa mapema;
2. Ilani ya kuhifadhi utaratibu; **na**
3. Ilani zinazohusiana na malalamiko ya mchakato unaotazamiwa.

RUHUSA YA MZAZI - UFAFANUZI

34 CFR §300.9

Ruhusa

Ruhusa inamaanisha:

1. Umejulishwa vikamilifu katika lugha yako ya asili au hali zingine za kuwasiliana (kama vile lugha ya ishara, Braili, au mawasiliano ya kusema) habari zote kuhusu hatua ambayo unapeana ruhusa.
2. Unaelewa na kukubali kwa kuandika hatua hiyo, na ruhusa hiyo inafafanua hatua hiyo na inaorodhesha rekodi (kama kuna yoyote) ambayo itatolewa na kwa nani; **na**
3. Unaelewa kwamba ruhusa hiyo ni ya kujitolea kwa sehemu yako na unaweza kuondoa ruhusa yako wakati wowote.

Ikiwa unataka kubatilisha (futa) ruhusa yako baada ya mtoto wako kuanza kupokea elimu maalum na huduma zinazoambatana, unapaswa kufanya hivyo kwa maandiko. Wewe kuondoa ruhusa haikanushi (kuondoa) hatua ambayo ilitekelezwa baada yako kupeana ruhusa na kabla ya wewe kuiondoa.Kwa kuongezea, shule ya wilaya haistahili kubadilisha (kugeuza) rekodi za elimu ya mtoto wako ili kuondoa marejeleo yoyote ambazo mtoto wako alipokea eliu maalum na huduma ziambatanazo baada ya kutoa ruhusa yako.

RUHUSA YA MZAZI

34 CFR §300.300

Ruhusa ya tathmini ya kwanza

Wilaya ya shule yako haiwezi kutekeleza tathmini ya kwanza ya mtoto wako ili kuamua kama mtoto wako anastahiki chini ya Sehemu B ya IDEA kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana bila ya kwanza kukupa ilani iliyoandikwa mapema ya hatua iliyopendekezwa na bila ya kupata ruhusa yako kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Ilani Iliyo Andikwa Awali na Ruhusa ya Mzazi.***

Wilaya ya shule yako ni lazima itie bidii ili kupata ruhusa yako unayoifahamu kwa ajili ya tathmini ya kwanza ili kuamua kama mtoto wako ni mtoto ambaye ana ulemavu.

Ruhusa yako ya tathmini ya kwanza haimaanishi kwamba umepeana pia ruhusa yako kwa wilaya ya shule kuanza kupeana elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako.

Ikiwa mtoto wako ameandikishwa katika shule ya umma au unatafuta kumwandikisha mtoto wako katika shule ya umma na umekataaa kupeana ruhusa au umeshindwa kujibu ombi la kupeana ruhusa ya tathmini ya kwanza, wilaya ya mtoto wako inaweza, lakini haipaswi, kutafuta kutekeleza tathmini ya kwanza ya mtoto wako kwa kutumia Sheria ya upatanisho au malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, mkutano wa suluhisho, na utaratibu wa kusikilizwa kwa mchakato adilifu unaotazamiwa (isipokuwa ikitakikana kufanywa hivyo au imekatazwa kufanywa hivyo chini ya sheria za Serikali). Wilaya ya shule yako haitakeuka uwajibikaji wake wa kumpata, kumtambua na kumtathmini mtoto wako kama haitafuata tathmini ya mtoto wako katika hali hizi, isipokuwa sheria za Serikali zinahitaji ifuate tathmini hio.

Sheria maalum za tathmini ya kwanza ya wanaolindwa na Serikali

Ikiwa mtoto analindwa na Serikali na haishi na wazazi wake —

Wilaya ya shule haitaji ruhusa ya tathmini ya kwanza kutoka kwa mzazi ili kuamua kama mtoto huyo ni mtoto mlemavu kama:

1. Licha ya jitihada za kufanya hivyo, wilaya ya shule haiwezi kumpata mzazi wa mtoto;
2. Haki za wazazi zimeondolewa kulingana na sheria za Serikali; **au**
3. Hakimu amepeana haki ya kufanya maamuzi ya kielimu na ruhusa ya tathmini ya kwanza kwa mtu ambaye si mzazi wa mtoto huyo.

Anayelindwa na Serikali, kama inavyotumiwa katika IDEA, inamaanisha mtoto ambaye, kama ilivyoamuliwa na Serikali ambayo mtoto huo anaishi, ni:

1. Mtoto wa kulea;
2. Anayeonekana analindwa na Serikali chini ya sheria za Serikali; **au**
3. Aliye katika ulinzi wa chombo cha umma cha maslahi ya watoto.

Kuna ondoleo moja unapaswa kujua Anayelindwa na Serikali haimjumuishi mtoto wa kulea ambaye ana mzazi wa kumlea *ambaye anaafikia fasili ya mzazi kama ilivyotumika katika IDEA*.

Ruhusa ya mzazi ya huduma

Wilaya ya shule yako ni lazima ipate ruhusa yako unayoifahamu kabla ya kupeana elimu maalum na huduma zinazolingana kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.

Wilaya ya shule yako ni lazima ijitahidi ili ipate ruhusa yako unayoifahamu kabla ya kupeana elimu maalum na huduma zinazolingana kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.

Usipojibu ombi la kupeana ruhusa yako kwa mtoto wako ili apokee elimu maalum na huduma zinazolingana kwa mara ya kwanza, au ukikataa kupeana ruhusa kama hiyo *au baadaye kubatilisha (futa) ruhusa yako kwa maandiko,* wilaya ya shule yako haitatumia kuhifadhi utaratibu (k.m upatanisho, malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, mkutano wa suluhisho, au utaratibu wa kusikilizwa kwa mchakato adilifu unaotazamiwa) ndiposa kupata makubaliano au uamuzi wa kuwa elimu hiyo maalum na huduma zinazohusiana (inayopendekezwa na Kikundi cha IEP cha mtoto wako) itapewa mtoto wako bila ya ruhusa yako.

Ukikataa kupeana ruhusa yako kwa mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma zinazolingana kwa mara ya kwanza, au usipojibu ombi la kupeana ruhusa kama hiyo *au baadaye kubatilisha (futa) ruhusa yako kwa maandiko* na wilaya ya shule haimpatii mtoto wako elimu maalum na huduma zinazolingana ambayo ilitafuta ruhusa yako kwa ajili yake, wilaya ya shule yako:

1. Haitakuwa imekeuka mahitaji ya kupeana elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) kwa mtoto kwa kukosa kwake kupeana huduma hizo kwa mtoto wako; **na**
2. Haihitajiki kuwa na mkutano wa mpango wa elimu ya kibinafsi (IEP) au kuanzisha IEP ya mtoto wako ya elimu maalum na huduma zinazo lingana ambayo ruhusa iliombwa kwa ajili yake.

Ikiwa utabatilisha (futa) ruhusa yako kwa maandiko kwa wakati wowote baada ya mtoto wako kwanza kupewa elimu maalum na huduma zinazo ambatana,, hapo shule ya wilaya huenda isiendelee kutoa huduma kama hizo, lakini ni lazima ikupe ilani iliyo andikwa awali, kama ilivyo elezwa chini ya kichwa ***Ilani iliyo Andikwa Awali,*** *kabla ya kusimamisha huduma hizo.*

Ruhusa ya mzazi ya kutathminiwa tena

Wilaya ya shule yako ni lazima ipate ruhusa yako unayoifahamu kabla ya kutathmini tena mtoto wako, isipokuwa wilaya ya mtoto wako inaweza kuonyesha kwamba:

1. Ilichukua hatua zinazofaa za kupata ruhusa yako ya kutathmini mtoto wako tena; **na**
2. Haukujibu.

Ukikataa kukubali mtoto wako atathminiwe tena, wilaya ya shule inaweza, lakini haitakikani, kufuatilia kutathminiwa tena kwa mtoto wako kwa kutumia upatanisho, malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, mkutano wa suluhisho, na utaratibu wa kusikilizwa kwa mchakato adilifu unaotazamiwa ili itafute kubadili kukataa kwako kupeana ruhusa ya mtoto wako kutathminiwa tena. Sawasawa na tathmini za kwanza, wilaya ya shule yako haitakuwa imekeuka uwajibikaji wake chini ya Sehemu B ya IDEA ikikataa kufuatilia tathmini tena katika njia hii.

Hati ya jitihada zinazofaa za kupata ruhusa ya mzazi

Shule yako ni lazima itunze hati za jitihada zinazofaa za kupata ruhusa ya mzazi ya tathmini za kwanza, za kupeana elimu maalum na huduma zinazolingana kwa mara ya kwanza, za kutathmini tena na kuwapata wazazi wa wanaolindwa na Serikali kwa tathmini za kwanza. Hati hiyo lazima iwe na rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule katika maeneo haya, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au zilizo jaribiwa kupigwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za mawasiliano zilizotumiwa wazazi na majibu yoyote yaliyopokewa; **na**
3. Rekodi za kina za ziara zilizofanywa kwa nyumba ya mzazi au mahali pa ajira na matokeo ya ziara hizo.

Mahitaji mengine ya ruhusa

Ruhusa yako haihitajiki kabla ya wilaya ya shule yako:

1. Kuhakiki data zilizomo kama sehemu ya tathmini ya mtoto wako au kutathmini tena; **au**
2. Kumpatia mtoto wako mtihani au tathmini nyingine ambayo inapewa watoto wote isipokuwa, kabla ya mtihani huo au tathmini, ruhusa inahitajika kutoka kwa wazazi wote wa watoto wote.

Wilaya ya shule yako haitatumia kukataa kwako kupeana ruhusa kwa huduma moja au shughuli ili kukunyima wewe au mtoto wako huduma zingine, manufaa, au shughuli.

Ikiwa umemwandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama yako mwenyewe au ikiwa unamfunza mtoto wako nyumbani, na haupeani ruhusa yako ya tathmini ya kwanza ya mtoto wako au mtoto wako kutathminiwa tena, au ulishindwa kujibu ombi la kupeana ruhusa yako, wilaya ya shule huenda isitumie utaratibu wake kutatua ghasia (k.v., upatanisho au malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, mkutano wa suluhisho, na utaratibu wa kusikilizwa kwa mchakato adilifu unaotazamiwa) na haihitajiki ili kumzingatia mtoto wako kama anayestahiki kupokea huduma za haki (huduma zinazopatikana kwa watoto walemavu wa shule ya kibinafsi waliyowekwa hapo na wazazi).

TATHMINI ZENYE KUJITEGEMA ZA KIELIMU

34 CFR §300.502

Kwa ujumla

Kama ilivyofafanuliwa hapo chini, una haki ya kupata tathmini yenye kujitegemea ya kielimu (IEE) kwa mtoto wako ikiwa haukubaliani na tathmini ya mtoto wako ambayo ilipatikana na wilaya ya shule yako.

Ukiomba tathmini yenye kujitegemea ya kielimu, wilaya ya shule ni lazima ikupe habari kuhusu ni wapi unaweza kupata tathmini yenye kujitegemea ya kielimu na kuhusu kanuni za wilaya ya shule ambayo hutumika kwa tathmini zenye kujitegemea za kielimu.

Ufafanuzi

Tathmini yenye kujitegemea ya kielimu ina maanisha tathmini inayo tekelezwa na mtahini anayestahiki ambaye hajaajiriwa na wilaya ya shule ambayo inauwajibikaji wa elimu ya mtoto wako.

Gharama ya umma inamaana kwamba wilaya ya shule italipa gharama yote ya tathmini au itahakikisha kwamba tathmini imetolewa bila malipo, kulingana na utoaji wa Sehemu B ya IDEA, ambayo uruhusu kila Serikali kutumia rasilimali yoyote ya Serikali, mitaa, Jimbo na kibinafsi ya usaidizi inayo patikana katika Serikali ili kufikia mahitaji ya Sheria ya Sehemu ya B.

Haki ya mzazi ya kutathmini kwa gharama ya umma

Una haki huru ya kutathmini elimuya mtoto wako kwa gharama ya umma ikiwa haukubaliani na tathmini ya mtoto wako ambayo ilipatikana na wilaya ya shule yako, chini ya masharti yanayofuata:

1. Ukiomba tathmini yenye kujitegemea ya kielimu kwa mtoto wako kwa gharama ya umma, wilaya ya shule yako lazima, bila kupoteza muda wowote, aidha: (a) Iwasilishe malalamiko ya mchakato unaotazamiwa ili kuomba kusikilizwa ili ionyeshe kwamba

mtoto wako anafaa; au (b) Itoe tathmini yenye kujitegemea ya kielimu kwa gharama ya umma, isipokuwa wilaya ya shule ionyeshe wakati wa kusikilizwa kwamba tathmini ya mtoto wako ambao ulipata haukufikia kanuni za wilaya ya shule.

2. Wilaya ya shule yako ikiomba kusikilizwa na uamuzi wa mwisho uwe kwamba tathmini ya mtoto wako ya wilaya ya shule yako inafaa, bado una haki ya tathmini yenye kujigemea ya kielimu, lakini sio kwa gharama ya umma.
3. Ukiomba tathmini yenye kijigemea ya kielimu kwa mtoto wako, wilaya ya shule inaweza kukuuliza ni kwanini unakataa tathmini ya mtoto wako iliyopatikana na wilaya ya shule yako. Walakini, wilaya ya shule yako haitahitaji ufafanuzi na haitapoteza wakati wa kutoa tathmini yenye kujigemea ya kielimu kwa mtoto wako kwa gharama ya umma au kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa ili kuomba kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa ili kulinda tathmini ya wilaya ya shule kwa mtoto wako.

Una haki ya tathmini moja tu yenye kujigemea ya kielimu kwa mtoto wako kwa gharama ya umma kila wakati wilaya ya shule yako inapotekeleza tathmini ya mtoto wako ambayo haukubaliani nao.

Tathmini zilizoanzishwa na mzazi

Ukipata tathmini yenye kujitegemea ya kibinafsi kwa mtoto wako kwa gharama ya umma au unaoshiriki pamoja na wilaya ya shule tathmini ya mtoto wako ambayo ulipata kwa gharama za kibinafsi:

1. Wilaya ya shule yako lazima izingatie matokeo ya tathmini ya mtoto wako, kama inafikia kanuni za wilaya ya shule ya tathmini zenye kujitegemea za kielimu, katika uamuzi wowote uliofanywa kulingana na utoaji wa elimu ya bure ya umma inayotakikana (FAPE) kwa mtoto wako; **na**
2. Wewe au wilaya ya shule yako inaweza kuleta tathmini hiyo kama ushahidi wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa kuhusu mtoto wako.

Maombi ya tathmini na maafisa wa kusikiza

Kama afisa wa kusikiza akiomba tathmini yenye kujitegemea ya kielimu kwa mtoto wako kama sehemu ya kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa, gharama ya tathmini ni lazima igharamiwe na umma.

Kanuni za wilaya ya shule

Ikiwa tathmini zenye kujitegemea ya kielimu ni kwa gharama ya umma, kanuni ambayo tathmini hiyo inapatikana, pamoja na eneo la tathmini na sifa zinazostahili za mtahini, lazima ziwe sawa na kanuni ambayo wilaya ya shule hutumia inapoanzisha tathmini (hadi kanuni hizo zilingane na haki yako ya tathmini yenye kujitegemea ya kielimu).

Isipokuwa kwa kanuni iliyofafanuliwa hapo juu, wilaya ya shule haiwezi kuweka masharti au muda maalum unaohusiana na kupata tathmini yenye kujitegemea ya kielimu kwa gharama ya umma.

USIRI WA HABARI

UFAFANUZI

34 CFR §300.611

Kama ilivyotumiwa chini ya kichwa cha **Siri za Habari:**

- *Uharibifu* unamaanisha uharibifu wa kimwili au kuondolewa kwa vitambulisho vya kibinafsi kutoka kwa habari ili habari hizo zisiweze kutambuliwa kibinafsi tena.
- *Rekodi za elimu* inamaanisha aina za rekodi zilizoshughulikiwa chini ya ufafanuzi wa "rekodi za elimu" katika 34 CFR sehemu ya 99 (maagizo yanayotekeleza Sheria ya Siri na Haki ya Elimu ya Jamii ya mwaka wa 1974, 20 U.S.C. 1232g (FERPA).
- *Chombo husika* inamaanisha wilaya yoyote ya shule, chombo au taasisi ambayo ukusanya, kutunza, au kutumia habari za mtu binafsi zinazoweza kutambuliwa, au kutoka kule habari zinapatikana, chini ya Sehemu B ya IDEA.

INAYOWEZA KUTAMBULIWA NA MTU BINAFSI

34 CFR §300.32

Inayoweza kutambuliwa na mtu binafsi inamaanisha habari ambazo zina:

(a) Jina la mtoto wako, jina lako kama mzazi, au jina la mtu mwingine wa familia;
(b) Anwani ya mtoto wako;
(c) Kitambulisho cha kibinafsi, kama vile namba ya mtoto wako ya usalama wa jamii au namba ya mwanafunzi; **au**
(d) Orodha ya tabia za kibinafsi au habari zingine ambazo zinawezesha kumtambua mtoto wako kwa uhakika.

ILANI KWA WAZAZI

34 CFR §300.612

Chombo cha Serikali cha Elimu ni lazima kipeane ilani ambayo inatosha kuwajulisha vikamilifu wazazi kuhusu siri ya habari za mtu binafsi zinazoweza kutambuliwa, pamoja na:

1. Ufafanuzi wa kadiri ambayo ilani hiyo inapeanwa katika lugha za asili za vikundi kadhaa vya umma katika Serikali;
2. Ufafanuzi wa watoto ambao habari zao za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa zinatunzwa, aina ya habari zinazotafutwa, mbinu ambazo Serikali inakusudia kutumia ili kukusanya habari hizo (pamoja na vyanzo ambavyo habari ukusanywa), na matumizi yatakayofanyiwa habari hizo;
3. Muhtasari wa sera na utaratibu ambao vyombo husika lazima zifuate kuhusu kuhifadhi, kufichua kwa chama cha tatu, uzuiaji, uharibifu wa habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa; **na**

4. Ufafanuzi wa haki zote za wazazi na watoto kuhusiana na habari hizi, pamoja na haki chini ya Sheria ya Siri na Haki ya Elimu ya Jamii (FERPA) na maagizo yake yanayotekeleza katika 34 CFR Sehemu ya 99.

Kabla ya shughuli yoyote kuu ya kutambua,kupata au kutathmini watoto walio na mahitaji ya elimu maalum na huduma zinazo ambatana (ijulikanayo pia kama "kumpata mtoto") ilani hiyo lazima ichapishwe au itangazwe kwenye gazeti au kwenye vyombo vingine vya habari, au zote, pamoja na mzunguko wa kutosha wa kuwajulisha wazazi katika Serikali yote juu ya matendo haya.

HAKI ZA UFIKIAJI

34 CFR §300.613

Chombo husika ni lazima kikuruhusu kuchunguza na kuhakiki rekodi zozote za kielimu zinazohusiana na mtoto wako ambazo zilizokusanywa, zilizotunzwa, au zilizotumiwa na wilaya ya shule yako chini ya Sehemu B ya IDEA. Chombo husika ni lazima kifuate ombi lako la kuchunguza na kuhakiki rekodi zozote za kielimu juu ya mtoto wako bila ya kupoteza wakati wowote na kabla ya mkutano wowote unaohusiana na mpango wa elimu ya kibinafsi (IEP), au kusikilizwa kwa mchakato adilifu unaotazamiwa (pamoja na mkutano wa suluhisho au kusikilizwa kunakohusiana na tabia), na katika hali yoyote isiwe zaidi ya siku 45 za kalenda baada ya ombi lako.

Haki yako ya kuchunguza na kuhakiki rekodi za kielimu inajumuisha:

1. Haki yako ya kujibiwa maombi yako ya maana juu ya ufafanuzi na utafsiri wa rekodi kutoka kwa chombo husika;
2. Haki yako ya kuomba kwamba chombo husika kitoe nakala za rekodi ikiwa hauwezi kuchunguza na kuhakiki vilivyo rekodi isipokuwa upokee nakala hizo; **na**
3. Haki yako ya mwakilishi wako kuchunguza na kuhakiki rekodi hizo.

Chombo husika kinaweza kudhania kwamba unaidhini ya kuchunguza na kuhakiki rekodi zinazohusiana na mtoto wako isipokuwa washauriwe kwamba hauna idhini chini ya sheria za Serikali zinazotumika zinazosimamia masuala kama hayo ya ulezi, au kuachana na talaka.

REKODI YA UFIKIAJI

34 CFR §300.614

Kila chombo husika ni lazima kitunze rekodi za vyama vinavyofikia rekodi za elimu zinazokusanywa, zinazotunzwa, au kutumiwa chini ya Sehemu B ya IDEA (isipokuwa wazazi na wafanyakazi walioidhinishwa wa chombo husika wanaofikia), pamoja na jina la chama, tarehe ambayo ufikiaji ulipeanwa, na kusudi la chama hicho kuidhinishwa kutumia rekodi hizo.

REKODI ZA ZAIDI YA MTOTO MMOJA

34 CFR §300.615

Ikiwa rekodi yoyote ya elimu ina habari ya zaidi ya mtoto mmoja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kuchunguza na kuhakiki habari zinazohusiana na watoto wao tu au kujulishwa habari hizo maalum.

ORODHA YA AINA NA MAENEO YA HABARI

34 CFR §300.616

Ikiombwa, kila chombo husika ni lazima kikupe orodha ya aina na maeneo ya rekodi za kielimu zilizokusanywa, zilizotunzwa, au kutumiwa na chombo hicho.

ADA

34 CFR §300.617

Kila chombo husika kinaweza kulipisha ada ya nakala za rekodi ambazo hukutengenezea chini ya Sehemu B ya IDEA, ikiwa ada hiyo haikuzuilii kutokana na kutekeleza haki yako ya kuchunguza na kuhakiki rekodi hizo.

Chombo husika kinaweza kukosa kulipisha ada ya kutafuta au kuchukua habari chini ya Sehemu B ya IDEA.

KUREKEBISHWA KWA REKODI MZAZI AKIOMBA

34 CFR §300.618

Ukiamini kwamba habari katika rekodi za elimu zilizokusanywa, kutunzwa, au kutumiwa kuhusu mtoto wako chini ya Sehemu B ya IDEA si sahihi, zinapotosha, au zinakeuka siri au haki zingine za mtoto wako, unaweza kuomba chombo husika ambacho kinatunza habari hizo kibadilishe habari hizo.

Chombo husika ni lazima kiamue aidha kubadilisha habari hizo kulingana na ombi lako kati ya kipindi cha muda unaoeleweka baada ya kupokea ombi lako.

Chombo husika kikikataa kubadilisha habari hizo kulingana na ombi lako, ni lazima kikujulishe juu ya katao hilo na kikushauri juu ya haki ya kusikilizwa kwa kusudi hili kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Nafasi ya Kusikilizwa.***

NAFASI YA KUSIKILIZWA

34 CFR §300.619

Chombo husika lazima, ikiombwa, kitoe nafasi ya kusikilizwa ili habari katika rekodi za elimu kuhusu mtoto wako zipingwe ili kuhakikisha kwamba ni sahihi, hazipotoshi, au kama sivyo hazikeuki siri au haki zingine za mtoto wako.

UTARATIBU WA KUSIKILIZWA

34 CFR §300.621

Kusikilizwa ili kupinga habari ndani ya rekodi za elimu lazima zitekelezwa kulingana na utaratibu wa kusikilizwa chini ya Sheria ya Siri na Haki za Elimu ya Jamii (FERPA).

MATOKEO YA KUSIKILIZWA

34 CFR §300.620

Ikiwa, kama matokea ya kusikilizwa, chombo husika kikiamua kwamba habari si sahihi, zinapotosha, au kama sivyo zinakeuka siri au haki zingine za mtoto, ni lazima kibadilishe habari hizo vilivyo na kikujulishe kwa kuandika.

Ikiwa, kama matokeo ya kusikilizwa, chombo husika kikiamua kwamba habari hizi si sahihi, zinapotosha, au kama sivyo zinakeuka siri au haki za mtoto, ni lazima kikujulishe juu ya haki yako ya kuweka katika rekodi hizo ambazo kinatunza juu ya mtoto wako taarifa ikitoa maoni juu ya habari hizo au ikitoa sababu zozote za kukataa uamuzi wa chombo husika.

Ufafanuzi kama huo unaowekwa katika rekodi za mtoto wako ni lazima:

1. Zitunzwe na chombo husika kama sehemu ya rekodi za mtoto wako maadamu rekodi hiyo au sehemu iliyokataliwa itunzwe na chombo husika; **na**
2. Chombo husika kikifichua rekodi za mtoto wako au sehemu iliyokataliwa kwa chama chochote, ufafanuzi lazima ufichuliwe kwa chama hicho pia.

RUHUSA YA KUFICHUA HABARI ZA KIBINAFSI ZINAZOWEZA KUTAMBULIWA

34 CFR §300.622

Isipokuwa habari hizo ziwe katika rekodi za elimu, na ufichuzi umeidhinishwa bila ruhusa ya mzazi chini ya sheria ya Siri na Haki ya Elimu ya Jamii (FERPA), ruhusa yako lazima ipatikane kabla ya habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa kufichuliwa kwa vyama kando na maafisa wa vyombo husika. Isipokuwa chini ya hali zilizoelezwa hapo chini, ruhusa yako haitakikani kabla ya habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa kufichuliwa kwa maafisa wa vyombo husika kwa makusudi ya kufikia mahitaji ya Sehemu B ya IDEA.

Ruhusa yako, au ruhusa ya mtoto anayestahiki ambaye amefikia umri wa wengi chini ya Sheria za Serikali, lazima ipatikane kabla ya habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa kufichuliwa kwa maafisa wa vyombo husika vinavyotoa au kulipia huduma za mabadiliko.

Ikiwa mtoto wako yuko, au anaenda shule ya kibinafsi ambayo haipo katika wilaya ya shule moja unayoishi, ruhusa yako lazima ipatikane kabla ya habari yoyote ya kibinafsi inayoweza kutambuliwa kuhusu mtoto wako kufichuliwa kati ya maafisa katika wilaya shule ambapo shule hiyo ya kibinafsi ipo na maafisa katika wilaya ya shule ambapo wewe unaishi.

KUHIFADHI

34 CFR §300.623

Kila chombo husika lazima kilinde siri ya habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa wakati wa kukusanywa, kutunzwa, kufichuliwa, na kuharibiwa.

Afisa mmoja kwa kila chombo husika lazima achukue uwajibikaji wa kuhakikisha siri ya habari zozote za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa.

Watu wote wanaokusanya au kutumia habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa lazima wapokee mafunzo au maagizo yanayohusiana na sera na utaratibu wa Serikali kuhusu siri chini ya Sehemu B ya IDEA na Sheria ya Siri na Haki ya Elimu ya Jamii (FERPA).

Kila chombo husika lazima kidumishe orodha mpya ya majina na vyeo vya wafanyakazi walio katika chombo hicho ambao wanaweza kufikia habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa ili umma iweze kuchunguza.

UHARIBIFU WA HABARI

34 CFR §300.624

Wilaya ya shule yako lazima ikujulishe wakati habari za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa ambazo zilikusanywa, zilitunzwa, au zilitumiwa hazihitajiki tena ili kutoa huduma za kielimu kwa mtoto wako.

Habari hizo lazima ziharibiwe wewe ukiomba. Walakini, rekodi ya kudumu ya jina la mtoto wako, anwani, na namba ya simu, gredi yake, rekodi ya kuhudhuria, darasa alizohudhuria, kiwango cha gredi aliyokamilisha, na mwaka aliyomaliza inaweza kutunzwa bila kizuizi cha wakati.

UTARATIBU WA MALALAMIKO YA SERIKALI

UTOFAUTI KATI YA MALALAMIKO YA KUSIKILIZWA KWA MCHAKATO UNAOTAZAMIWA NA UTARATIBU WA MALALAMIKO YA SERIKALI

Maagizo ya Sehemu B ya IDEA imeweka utaratibu tofauti wa Malalamiko ya Serikali na malalamiko ya mchakato unaotazamiwa na kusikilizwa. Kama ilivyofafanuliwa hapo chini, mtu yeyote au shirika lolote linaweza kuwasilisha malalamiko ya Serikali kwa kudai ukeukaji wa mahitaji ya Sehemu yoyote ya B na wilaya ya shule, Chombo cha Elimu cha Serikali, au chombo chochote cha umma. Ni wewe tu au wilaya ya shule inaweza kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa juu ya suala lolote linalohusiana na pendekezo au kutoanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini au mahali pa elimu ya mtoto mlemavu, au utoaji wa elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) kwa mtoto. Ijapokuwa Wafanyakazi wa Chombo cha Elimu cha Serikali kwa ujumla lazima watatue malalamiko ya Serikali kati ya muda maalum wa siku 60 za kalenda, isipokuwa muda huo maalum uongezwe vizuri, afisa wa kusikiliza mchakato adilifu unaotazamiwa lazima asikilize malalamiko ya mchakato unaotazamiwa (ikiwa haujatatuliwa

kupitia mkutano wa suluhisho au kupitia mapatano) na apeane uamuzi ulioandikwa kati ya siku 45 za kalenda baada ya mwisho wa kipindi cha suluhisho, kama ilivyofafanuliwa kwenye hati hii chini ya kichwa cha Mchakato wa Suluhisho, isipokuwa afisa wa kusikiza aongeze muda maalum wewe ukiomba au wilaya ya shule ikiomba. Malalamiko ya Serikali na malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, utaratibu wa suluhisho na kusikilizwa yamefafanuliwa zaidi hapo chini.*Ajenti wa Elimu ya Taifa ni lazima iunde mifano ya miundo ili kukusaidia kuweka kesi kwa utaratibu wa malalamishi unaotazamiwa na kukusaidia wewe au wana chama wengine kuweka kesi ya Malalamishi ya Taifa kama ilivyo katika kichwa* ***Mifano ya Miundo.***

KUCHUKULIWA KWA UTARATIBU WA MALALAMIKO YA SERIKALI

34 CFR §300.151

Kwa ujumla

Kila Chombo cha Elimu cha Serikali lazima kiwe na utaratibu ulioandikwa wa:

1. Kutatua malalamiko yoyote, pamoja na malalamiko yaliyowasiishwa na shirika au mtu kutoka Jimbo lingine;
2. Kuwasilishwa kwa malalamiko na Chombo cha Elimu cha Serikali;
3. Kusambaza zaidi utaratibu wa malalamiko ya Serikali kwa wazazi na watu wengine wanaopendezwa, pamoja na vituo vya habari na vya kuwafunza wazazi, vyombo vya ulinzi na uwakili, vituo vya kuishi vyenye kujitegemea, na vitu vingine vinavyofaa.

Marekebisho ya kunyimwa huduma muhimu

Katika kutatua malalamiko ya Serikali ambayo Chombo cha Elimu cha Serikali kimepata ukosefu wa kutoa huduma muhimu, Chombo cha Elimu cha Serikali lazima kishughulikie:

1. Ukosefu wa kutoa huduma muhimu, pamoja na hatua sahihi muhimu ya kushughulikia mahitaji ya mtoto *(kama huduma za fidia au kulipia fedha);* **na**
2. Utoaji muhimu wa usoni wa huduma kwa watoto wote walemavu.

UTARATIBU WA CHINI WA MALALAMIKO YA SERIKALI

34 CFR §300.152

Kizuizi cha wakati; Utaratibu wa chini

Kila Chombo cha Elimu cha Serikali lazima kijumuishe katika utaratibu wake wa malalamiko ya serikali kizuizi cha wakati wa siku 60 za kalenda baada ya malalamiko kuwasilishwa ili:

1. Kitekeleze uchunguzi wenye kujitegemea wa mahali hapo, ikiwa Chombo cha Elimu cha Serikali kikiamua kwamba uchunguzi ni muhimu;
2. Kumpa mwenye kulalamika nafasi ya kuwasilisha habari zaidi, aidha kwa kusema au kwa kuandika, kuhusu madai kwenye malalamiko;
3. Kupatia wilaya ya shule au chombo kingine cha umma nafasi ya kujibu malalamiko, pamoja na; (a) kwa chaguo la chombo; pendekezo la kutatua malalamiko; **na** (b) nafasi

ya mzazi kuwasilisha malalamiko na chombo kukubali kwa kujitolea kujihusisha katika mapatano:

4. Kuhakiki habari zote muhimu na kufanya uamuzi wa kibinafsi wa kama wilaya ya shule au chombo kingine cha umma kinakeuka mahitaji ya Sehemu B ya IDEA; **na**
5. Kupeana uamuzi ulioandikwa kwa mwenye kulalamika ambao unashughulikia madai kwenye malalamiko na inayojumuisha: (a)kweli na hitimisho iliyopatikana ; **na** (b) sababu za uamuzi wa mwisho wa Chombo cha Elimu cha Serikali.

Muda kuongezwa; uamuzi wa mwisho; utekelezaji

Utaratibu wa chombo cha Elimu cha Serikali uliofafanuliwa hapo juu lazima pia:

1. Iruhusu kuongezwa kwa kizuizi cha wakati wa siku 60 tu za kalenda ikiwa: (a) hali za kipekee ziliopo kulingana na malalamiko ya Serikali maalum; **au** (b) wazazi na wilaya ya shule au chombo kingine cha umma kinachohusika kwa kujitolea kikubali kuongeza muda wa kutatua suala hilo kupitia upatanisho au njia zingine za kutatua mzozo, ikiwa inapatikana katika Serikali.
2. Ijumuishe utaratibu wa utekelezaji kamili wa uamuzi wa mwisho wa Chombo cha Elimu cha Serikali, ikitakikana, pamoja na: (a) shughuli za usaidizi wa kiufundi; (b) majadiliano; **na** (c) hatua sahihi za kufikia masharti.

Malalamiko ya serikali na kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa

Malalamiko ya Serikali yaliyoandikwa yakipokewa ambayo pia ni suala la kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa kama ilivyofafanuliwa hapo chini chini ya kichwa cha ***Kuwasilisha Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa***, au malalamiko ya Serikali yanajumuisha masuala kadhaa ambayo moja au zaidi ni sehemu ya kusikilizwa kama huko, Serikali lazima iweke kando malalamiko ya Serikali, au sehemu yoyote ya malalamiko ya Serikali ambayo yanashughulikiwa katika kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa hadi kusikilizwa huko kuishe. Suala lolote katika malalamiko ya Serikali ambayo sio sehemu ya kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa lazima itatuliwe kwa kutumia kizuizi cha wakati na utaratibu uliofafanuliwa hapo juu.

Suala likizuka katika malalamiko ya Serikali ambalo liliamuliwa hapo awali katika kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa ikijumuisha vyama vile vile (wewe na wilaya ya shule), kisha uamuzi wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa uwe wa kubana kwa suala hilo na Chombo cha Elimu cha Serikali lazima kimjulishe mwenye kulalamika kwamba uamuzi ni wa kubana.

Malalamiko yanayodai wilaya ya shule au chombo kingine cha umma kilikosa kutekeleza uamuzi wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa lazima yatatuliwe na Chombo cha Elimu cha Serikali.

KUWASILISHA MALALAMIKO YA TAIFA

34 CFR §300.153

Shirika au mtu anaweza kuwasilisha Malalamiko ya Serikali yaliyoandikwa na kutiwa saini chini ya utaratibu uliofafanuliwa hapo juu.

Malalamiko ya Serikali lazima yajumuishe:

1. Taarifa ya kwamba wilaya ya shule au chombo kingine cha umma kimekeuka hitaji la Sehemu B ya IDEA au kutekeleza kanuni yake katika 34 CFR Sehemu ya 300;
2. Ukweli wa msingi wa taarifa hii;

3. Saini na habari ya mawasiliano ya mwenye kuwasilisha malalamiko; na
4. Ikiwa unadai ukeukaji kuhusu mtoto fulani:
   (a) Jina la mtoto na anwani ya makao ya mtoto huyo;
   (b) Jina la shule ambayo mtoto uhudhuria;
   (c) Katika hali ya mtoto au kijana asiye na makao, habari ya anwani ya mtoto huyo, na jina ya shule ambayo mtoto huyo anahudhuria;
   (d) Ufafanuzi wa hali ya shida ya mtoto, pamoja na kweli zinazohusiana na shida hiyo; **na**
   (e) Suluhisho iliyopendekezwa ya shida hiyo na vile inavyojulikana na kupatikana kwa chama kinachowasilisha malalamiko hayo wakati malalamiko yalipowasilishwa.

Malalamiko hayo lazima yadai ukeukaji uliofanyika zaidi ya mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo malalamiko yalipokewa kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Kuchukuliwa kwa Utaratibu wa Malalamiko ya Serikali.***

Chama kinachowasilisha malalamiko lazima kipeleke mbele nakala ya malalamiko kwa wilaya ya shule au chombo kingine cha umma kinachohudumia mtoto huyo kwa wakati mmoja ambao chama hicho kinawasilisha malalamiko hayo kwa Chombo cha Elimu cha Serikali.

HARAKATI YA UTARATIBU WA MALALAMIKO UNAOTAZAMIWA

KUWASILISHA MALALAMIKO YA MCHAKATO UNAOTAZAMIWA

34 CFR §300.507

Kwa ujumla

Wewe au wilaya ya shule inaweza kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa juu ya suala lolote linalohusiana na pendekezo au kutoanzisha au kubadilisha kitambulisho, tathmini au mahali pa elimu ya mtoto wako, au utoaji wa elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) kwa mtoto.

Malalamiko ya mchakato unaotazamiwa lazima udai ukeukaji ambao ulitendeka baada ya miaka miwili kabla wewe au wilaya ya shule ilijua au ilipaswa kujua kuhusu hatua iliyodaiwa ambayo uunda msingi wa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa.

Muda maalum ulio hapo juu hautumiki ikiwa hauwezi kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa kati ya muda maalum kwa sababu:

1. Wilaya ya shule haswa ilitafsiri vibaya kwamba ilikuwa imetatua masuala yaliyotambuliwa kwenye malalamiko; **au**
2. Wilaya ya shule ilikuficha habari ambazo ilipaswa kukupa chini ya Sehemu B ya IDEA.

Habari kwa wazazi

Wilaya ya shule lazima ikujulishe kuhusu huduma zozote muhimu za bure za kisherea au za gharama ya chini zinazopatikana katika eneo ikiwa utaomba habari hizo, **au** wewe au wilaya ya shule ikiwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa.

MALALAMIKO YA MCHAKATO UNAOTAZAMIWA

34 CFR §300.508

Kwa ujumla

Ndiposa kuomba kusikilizwa, wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) lazima awasilishe malalamiko ya mchakato unaotazamiwa kwa chama kile kingine. Malalamiko hayo lazima yajumuishe yote yaliyomo yaliyoorodheshwa na lazima yawekwe siri.

Wewe au wilaya ya shule, yoyote aliyewasilisha malalamiko hayo, lazima pia apatie Chombo cha Elimu cha Serikali nakala ya malalamiko.

Yaliyomo kwenye malalamiko

Malalamiko ya mchakato unaotazamiwa lazima yajumuishe:

1. Jina la mtoto;
2. Anwani ya makao ya mtoto;
3. Jina la shule ya mtoto;
4. Ikiwa mtoto ni mtoto au kijana ambaye hana makao, habari za mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto;
5. Ufafanuzi wa hali ya shida ya mtoto inayo husiana na hatua iliyo pendekezwa au kukataliwa, pamoja na kweli zinazohusiana na shida hiyo; **na**
6. Suluhisho iliyo pendekezwa ya shida hiyo na vile inavyojulikana na kupatikana kwa mhusika anaye lalamika (wewe au au wilaya ya shule) kwa wakati huo.

Ilani inayohitajika kabla ya kusikilizwa kwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa

Wewe au wilaya ya shule mwaweza kukosa kupata kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa hadi wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule), awakilishe malalamiko ya mchakato unaotazamiwa ambao unajumuisha habari zilizoorodheshwa hapo juu.

Utoshelevu wa malalamiko

Ndiposa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa yaendelee mbele, lazima yaonekane kwamba yanatosha. Malalamiko ya mchakato unaotazamiwa yataonekana yakutosha (yatakuwa yamefikia mahitaji ya yaliyomo hapo juu) isipokuwa chama kinachopokea malalamiko ya mchakato unaotazamiwa (wewe au wilaya ya shule) kimjulishe afisa wa kusikiliza na chama kile kingine kwa kuandika, kati ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko hayo, ya kwamba chama kinachopokea kinaamini kwamba malalamiko ya mchakato unaotazamiwa haufikii mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu.

Kati ya siku tano za kalenda baada ya kupokea taarifa, chama kinachopokea (wewe au wilaya ya shule) kitaonelea malalamiko ya mchakato unaotazamiwa kuwa hayatoshi, afisa wa kusikiliza lazima amue kama malalamiko ya mchakato unaotazamiwa yanafikia mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu, na akuarifu wewe na wilaya ya shule kwa kukuandikia mara moja.

Kurekebishwa kwa malalamiko

Wewe au wilaya ya shule inaweza kufanya mabadiliko kwa malalamiko kama tu:

1. Chama kile kingine kikiidhinisha mabadiliko kwa kuandika na kimepewa nafasi ya kutatua malalamiko ya mchakato unaotazamiwa kupitia mkutano wa suluhisho, uliofafanuliwa chini *ya kichwa cha **Harakati ya Suluhisho***; **au**

2. Isipite siku tano kabla ya kuanza kwa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa, afisa wa kusikiliza apeane ruhusa ya mabadiliko hayo.

Ikiwa chama kinacholalamika (wewe au wilaya ya shule) kikifanya mabadiliko kwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, muda maalum wa mkutano wa suluhisho (kati ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko) na kipindi cha muda wa suluhisho (kati ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea malalamiko) huanza tena siku ile malalamiko yaliyorekebishwa huwasilishwa.

Majibu ya chombo cha elimu cha mtaani (LEA) au wilaya ya shule kwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa.

Ikiwa wilaya ya shule haijakutumia ilani iliyoandikwa mapema, kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Ilani Iliyoandikwa Mapema***, kuhusu suala kuu katika malalamiko yako ya mchakato unaotazamiwa, wilaya ya shule lazima, kati ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, ikutumie majibu ambayo yanajumuisha:

1. Ufafanuzi wa kwanini wilaya ya shule ilipendekeza au ilikataa kuchukua hatua iliyoletwa katika malalamiko ya mchakato unaotazamiwa;
2. Ufafanuzi wa chaguzi zingine ambazo Kikundi cha mpango wa elimu ya kibinafsi ya mtoto wako (IEP) kilionelea na sababu ambazo chaguzi hizo zilikataliwa;
3. Ufafanuzi wa kila utaratibu wa tathmini, uchunguzi, rekodi au ripoti ambayo wilaya ya shule yako ilitumia kama msingi wa hatua iliyopendekezwa au kukataliwa; **na**
4. Ufafanuzi wa hali zingine ambazo ni muhimu kwa hatua iliyopendekezwa au kukataliwa ya wilaya ya shule.

Kutoa habari kwenye vipengele 1-4 hapo juu haizuii wilaya ya shule kutokana na kusisitiza kwamba malalamiko yako ya mchakato unaotazamiwa haukutosha.

Majibu ya chama kingine kwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa

Isipokuwa kama ilivyosemwa chini ya kichwa-kidogo juu ya, ***Majibu ya chombo cha elimu cha mtaani (LEA) au wilaya ya shule kwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa***, chama kinachopokea malalamiko ya mchakato unaotazamiwa lazima, kati ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea malalamiko, kitumie chama kile kingine majibu ambayo yanahutubia haswa masuala kwenye malalamiko hayo.

FOMU ZA MFANO

34 CFR §300.509

Chombo cha Elimu cha Serikali kimeanzisha fomu za mfano ili kukusaidia wewe kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa na *kukusaidia wewe na wahusika wengine kuwasilisha malalamiko ya Serikali. Walakini, Serikali yako au wilaya ya shule huenda isihitaji matumizi ya fomu hizi za mfano.* Kwa kweli, unaweza kutumia mfano wa fomu hiii au fomu nyingine inayofaa, maadamu ina habari zinazohitajika za kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa au malalamiko ya Serikali. Ili upate fomu za mfano unaweza kufanya yanayofuata:

1. Pakua kutoka kwa tovuti hii – http://www.dese.mo.gov/divspeced/Complaint_System/index.htm
2. Pigia simu Idara ya Missouri ya Elimu ya Msingi na ya Upili, nambari ya simu (573) 751-0602.

UPATANISHO

34 CFR §300.506

Kwa ujumla

Chombo cha Elimu cha Serikali lazima kifanye upatanisho upatikane ili wewe na wilaya ya shule iruhusiwe kutatua mizozo inayohusiana na suala lolote chini ya Sehemu B ya IDEA, pamoja na masuala yanayotokea baada ya kuwasilishwa kwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa. Hivyo basi, upatanisho unapatikana ili kutatua mizozo chini ya Sehemu B ya IDEA, iwe umewasilisha au haujawasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa ili kuomba kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Kuwasilisha Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa.***

Mahitaji

Utaratibu lazima uhakikishe kwamba mchakato wa upatanisho:

1. Ni wa kujitolea kwa upande wako na kwa upande wa wilaya ya shule;
2. Haujatumiwa kukunyima au kucheleweshe haki yako ya kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa, au kukataa haki zingine zozote ambazo unazo chini ya Sehemu B ya IDEA; **na**
3. Umetekelezwa na mpatanishaji aliyehitimu na asiye na upendeleo ambaye amefunzwa kuhusu mbinu kamili za upatanisho.

Ili kuomba upatanisho tuma ombi lililoandikwa kwa:

Missouri Department of Elementary and Secondary Eduation
Division of Special Education/Compliance Section
PO Box 480
Jefferson City, MO 65102-0480

Wilaya ya shule inaweza kuanzisha utaratibu ambao unawapa wazazi na shule ambazo zinachagua kutotumia mchakato wa upatanisho, nafasi ya kupatana, kwa wakati na mahali panapofaa kwako, na chama ambacho ni cha haki:

1. Ambaye amebanwa na kandarasi na chombo kingine maalum cha kutatua mzozo, au kituo cha habari na cha kuwafunza wazazi au kituo cha habari cha wazazi wa jamii katika Serikali; **na**
2. Ambaye atafafanua manufaa na akuimize utumie mchakato wa upatanisho.

Serikali lazima iwe na orodha ya watu ambao ni wapatanishaji waliohitimu na wanaojua sheria na masharti yanayohusiana na toleo la elimu maalum na huduma zinazolingana. Chombo cha Elimu cha Serikali lazima kiwachague wapatanishaji kwa mpangilio usio na utaratibu, kwa kuzunguka, au njia zingine za haki.

Serikali inauwajibikaji wa gharama ya mchakato wa upatanisho, pamoja na gharama za mikutano.

Kila mkutano katika mchakato wa upatanisho lazima upangwe kwa njia ya muda na ufanywe mahali panapofaa kwako na wilaya ya shule.

Wewe na wilaya ya shule mkitatua mzozo kupitia mchakato wa upatanisho, vyama vyote lazima viingie kwa makubaliano ya kisheria yanayobana ambayo yanaorodhesha suluhisho hilo na:

1. Inayosema kwamba majadiliano yote yaliyofanywa wakati wa mchakato wa upatanisho utabakia siri na hauwezi kutumiwa kama ushahidi katika kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa au kesi ya umma *(kesi ya mahakama);* **na**
2. Imetiwa saini na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye anaidhini ya kubana wilaya ya shule.

Makubaliano yaliyoandikwa, na kutiwa saini yanaweza kulazimishwa katika korti yoyote ya Serikali yenye mamlaka ya kisheria (korti ambayo inamamlaka ya kusikiliza kesi ya aina hii chini ya sheria za Serikali) au katika korti ya wilaya ya Marekani.

Majadiliano ambayo yalifanyika wakati wa mchakato wa upatanisho lazima yawe siri. Hayawezi kutumiwa kama ushahidi katika kusikilizwa kwowote kwa usoni kwa mchakato unaotazamiwa au kesi ya umma ya korti yoyote ya Jimbo au korti ya Serikali ya Jimbo linalopokea usaidizi chini ya Sehemu B ya IDEA.

Uadilifu wa mpatanishaji

Mpatanishaji huyo:

1. Hawezi kuwa mfanyakazi wa Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule ambayo inahusika katika elimu au ulezi wa mtoto wako; **na**
2. Lazima asiwe na upendeleo wa kibinafsi au wa kikazi ambao unazozana na madhumuni ya mpatanishaji.

Mtu ambaye anahitimu kama mpatanishaji si mfanyakazi wa wilaya ya shule au chombo cha Serikali kwa sababu yeye analipwa na chombo au wilaya ya shule ili ahudumu kama mpatanishaji.

MCHAKATO WA SULUHISHO

34 CFR §300.510

Mkutano wa suluhisho

Kati ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea ilani yako ya malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, na kabla ya kuanza kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa, wilaya ya shule lazima iite mkutano kati yako na wanachama wanaofaa wa Kikundi cha mpango wa elimu ya kibinafsi (IEP) ambao wanaufahamu maalum wa kweli zilizotambuliwa katika malalamiko yako ya mchakato unaotazamiwa. Mkutano huo:

1. Lazima uwe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye anamlaka ya kufanya uamuzi kwa niaba ya wilaya ya shule; **na**
2. Hauwezi kuwa na wakili wa wilaya ya shule isipokuwa wewe umezindikishwa na wakili.

Wewe na wilaya ya shule muamue wanachama wanaofaa wa Kikundi cha IEP watakaohudhuria mkutano huo.

Madhumuni ya mkutano huo ni wewe ujadili malalamiko yako ya mchakato unaotazamiwa, na kweli ambazo zinaunda msingi wa malalamiko hayo, ili wilaya ya shule iwe na nafasi ya kutatua mzozo huo.

Mkutano huo wa suluhisho sio lazima ikiwa:

1. Wewe na wilaya ya shule mkikubaliana kwa kuandika kuondoa mkutano huo; **au**
2. Wewe na wilaya ya shule mkikubaliana kutumia njia ya upatanisho, kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Upatanisho.***

Kipindi cha suluhisho

Ikiwa wilaya ya shule haijatatua malalamiko ya mchakato unaotazamiwa hadi ukaridhika kati ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea malalamiko ya mchakato unaotazamiwa (wakati wa kipindi cha muda wa mchakato wa suluhisho) kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa unaweza kufanywa.

Muda maalum wa siku 45 za kalenda wa kutoa uamuzi wa mwisho wa kusikiwa kwa mchakato unao tazamiwa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Uamuzi wa Kusikiliza*** huanza baada ya kuisha kwa siku 30 za kalenda za kipindi cha suluhisho, na ruhusa zingine za marekebisho yaliyofanywa kwa siku 30 za kalenda za kipindi cha suluhisho, kama ilivyofafanulia hapo chini.

Isipokuwa mahali ambapo wewe na wilaya ya shule mmekubaliana kuondoa mchakato wa suluhisho au kutumia upatanisho, kukosa kwako kuhusika katika mkutano wa suluhisho kunaweza kucheleweshe muda maalum wa mchakato wa suluhisho na kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa hadi mkutano ufanywe.

Ikiwa baada ya kufanya jitihada na kuandika jitihada hizo, wilaya ya shule haiwezi kukupata katika mkutano wa suluhisho, wilaya ya shule inaweza, wakati wa mwisho wa siku 30 za kalenda za kipindi cha suluhisho, kuomba kwamba afisa wa kusikiliza atupilie mbali malalamiko yako ya mchakato unaotazamiwa. Kuandikwa kwa jitihada kama hizo lazima kujumuishe rekodi ya majaribo ya wilaya ya shule kupanga wakati na mahali mnapokubaliana wote, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au zilizojaribiwa kupigwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za mawasiliano ulizotumiwa na majibu yoyote yaliyopokewa; **na**
3. Rekodi za kina za ziara zilizofanywa kwa nyumba yako au mahali pa ajira na matokeo ya ziara hizo.

Ikiwa wilaya ya shule ikikosa kufanya mkutano wa suluhisho kati ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea ilani yako ya malalamiko ya mchakato unaotazamiwa **au** ikose kuhusika kwenye mkutano wa suluhisho, unaweza kumuuliza afisa wa kusikiliza *aanzishe wakati wa mchakato wa kusikizwa unao tazamiwa wa siku 45-kalenda.*

Marekebisho ya siku 30 za kalenda za kipindi cha suluhisho

Wewe na wilaya ya shule mkikubali kwa kuandika kuondoa mkutano wa suluhisho, basi muda maalum wa siku 45 za kalenda za kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa huanza siku inayofuata.

Baada ya kuanza kwa upatanisho au mkutano wa suluhisho na kabla ya mwisho wa siku 30 za kalenda za kipindi cha suluhisho, wewe na wilaya ya shule mkikubali kwa kuandika kwamba hakuna makubaliano yanayo wezekana, basi muda maalum wa siku 45 za kalenda za kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa huanza siku inayofuata.

Wewe na wilaya ya shule mkikubali kutumia mchakato wa upatanisho lakini bado haija fikia mapatano, wakati wa mwisho wa siku 30 za kalenda za kipindi cha suluhisho, mchakato wa upatanisho huenda ikaendelezwa hadi makubaliano yapatikane ikiwa wahusika watakubaliana kwa kuendeleza kwa maandiko.Walakini, wewe au wilaya ya shule mkijiondoa kutoka kwa mchakato wa upatanisho, basi muda maalum wa siku 45 za kalenda wa kusikilizwa kwa mchakato unao tazamiwa huanza siku inayofuata.

Makubaliano yaliyoandikwa ya mahali

Suluhisho la mzozo likifikiwa katika mkutano wa suluhisho, wewe na wilaya ya shule lazima muingie katika makubaliano ya kisheria yanayobana ambayo:

1. Yametiwa saini na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye anaidhini ya kubana wilaya ya shule; **na**
2. Yanaweza kulazimishwa katika korti yoyote ya Serikali yenye mamlaka ya kisheria (korti ambayo inamamlaka ya kusikiliza kesi ya aina hiyo) au katika korti ya wilaya ya Marekani au na Chombo cha Elimu cha Serikali, ikiwa Jimbo lako halina mbinu nyingine au utaratibu mwingine ambao unaruhusu vyama kutafuta kulazimishwa kwa makubaliano ya suluhisho.

Kipindi cha kuhakiki makubaliano

Wewe na wilaya ya shule mkiingia katika makubaliano kama matokeo ya mkutano wa suluhisho, nyinyi wote (wewe au wilaya ya shule) mnaweza kubatilisha makubaliano hayo kati ya siku 3 za biashara baa ya wakati wewe na wilaya ya shule mlitia saini makubaliano hayo.

HARAKATI YA KUSIKILIZWA KWA MALALAMISHI INAYOTAZAMIWA

KUSIKILIZWA KWA MCHAKATO ADILIFU UNAOTAZAMIWA

34 CFR §300.511

Kwa ujumla

Wakati wowote malalamiko ya mchakato unaotazamiwa yanapowasilishwa, wewe au wilaya ya shule inayohusika katika mzozo huu lazima mpate nafasi ya kusikilizwa kwa mchakato adilifu unaotazamiwa, kama ilivyofafanuliwa katika sehemu za ***Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa*** na ***Mchakato wa Suluhisho***.

Ombi lililoandikwa la kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa lazima litumwe kwa Idara ya Missouri ya Elimu ya Msingi na ya Upili, na lazima nakala itolewe na itumwe kwa chombo ambacho unaanzisha mchakato unaotazamiwa dhidi yake.

Anwani ya kutuma barua ya Idara hiyo ni:

MODESE
Attention: Compliance Section/Special Education
PO Box 480
Jefferson City, MO 65102
Faksi: (573) 526-4404

Afisa mwadilifu wa kusikiliza

Kwa uchache, afisa wa kusikiliza:

1. Lazima asiwe mfanyakazi wa Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule ambayo inahusika katika elimu au ulezi wa mtoto huyo. Walakini, mtu si mfanyakazi wa chombo kwa sababu yeye analipwa na chombo hicho ili kuhudumu kama afisa wa kusikiliza;
2. Lazima asiwe na upendeleo wa kibinafsi au wa kikazi ambao unazozana na madhumuni ya afisa wa kusikiliza wakati wa kusikilizwa.
3. Lazima awe anafahamu na kuelewa toleo za IDEA, na maagizo ya Jimbo na Serikali kuhusu IDEA, na ukalimani wa kisheria wa IDEA na korti za Jimbo na Serikali; **na**
4. Lazima awe na ufahamu na uwezo wa kutekeleza kusikilizwa, na kufanya na kuandika maamuzi, yanayo ambatana na zoezi linalofaa la kawaida la kisheria.

Kila wilaya ya shule lazima iweke orodha ya watu wale ambao wanahudumu kama maafisa wa kusikiliza ambayo inajumuisha taarifa ya sifa zinazostahili za kila afisa wa kusikiliza.

Suala kuu la kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa

Upande ambao unaomba kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa (wewe au wilaya ya shule) hauwezi kuleta masuala wakati wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa ambao haukushughulikiwa katika malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, isipokuwa upande ule mwingine ukubali.

Muda maalum wa kuomba kusikilizwa

Wewe au wilaya ya shule lazima iombe kusikilizwa adilifu juu ya malalamiko ya mchakato unaotazamiwa kati ya miaka miwili ya tarehe wewe au wilaya ya shule ilipojua au ilipaswa kujua kuhusu suala lililoshughulikiwa kwenye malalamiko.

Kinzano za muda maalum

Muda maalum ulio hapo juu hautumiki ikiwa haukuweza kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa kwa sababu:

1. Wilaya ya shule haswa ilitafsiri vibaya kwamba ilikuwa imetatua shida au suala ambalo unaleta katika malalamiko yako; **au**
2. Wilaya ya shule ilikuficha habari ambazo ilipaswa kukupa chini ya Sehemu B ya IDEA.

HAKI ZA KUSIKILIZWA

34 CFR §300.512

Kwa ujumla

Una haki ya kujiwakilisha mwenyewe wakati wa kuzikilizwa wa mchakato unaotazamiwa. Kuongezea hayo upande wowote wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa (pamoja na kusikilizwa kunako husiana na utaratibu wa kufunza nidhamu) una haki ya:

1. Kuzindikishwa na kushauriwa na wakili au watu walio na ufahamu maalum au mafunzo kuhusu shida za watoto walemavu;
2. Kuwakilishwa wakati wa mchakato unaotazamiwa na wakili;
3. Ushahidi wa sasa na kukabili, kuchunguza, na kuhitaji washahidi wahudhurie;

4. Kukataa kuletwa kwa ushahidi wowote wakati wa kusikilizwa ambao haujafichuliwa kwa chama hicho kabla ya siku tano za biashara kabla ya kusikilizwa;
5. Kupata rekodi iliyoandikwa ya kusikilizwa ya neno baada ya neno, au, kwa chaguo lako, ya elektroniki, **na**
6. Kupata matokeo ya kweli na maamuzi yaliyoandikwa, au, kwa chaguo lako, ya elektroniki.

Ufichuaji zaidi wa habari

Kwa uchache siku tano za biashara kabla ya kusikilizwa kwa mchakato unaotaziwa, wewe na wilaya ya shule lazima mfichue kwa yule mwingine tathmini zote zilizokamilika kabla ya tarehe hiyo na mapendekezo ambayo msingi wake ni tathmini hiyo ambayo wewe au wilaya ya shule mnakusudia kutumia wakati wa kusikilizwa.

Afisa wa kusikiliza anaweza kuzuia chama chochote ambacho kinashindwa kufuata hitaji hili kutokana na tathmini inayofaa au mapendekezo wakati wa kusikilizwa bila ruhusa ya chama kile kingine.

Haki za mzazi wakati wa kusikilizwa

Lazima upewe haki ya:

1. Mtoto wako kuwepo;
2. Kufungua kusikilizwa kwa umma; **na**
3. Kupewa rekodi ya kusikilizwa, matokeo ya kweli na maamuzi bila gharama yoyote.

MAAMUZI YA KUSIKILIZWA

34 CFR §300.513

Uamuzi wa afisa wa kusikiliza

Uamuzi wa afisa wa kusikiliza wa kama mtoto wako alipokea elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) lazima msingi wake uwe misingi ya ushahidi na mabishano ambayo moja kwa moja inaambatana na FAPE..

Katika hoja zinazodai ukiukaji wa utaratibu *(kama vile 'Timu isiyokamilika ya IEP"),* afisa wa kusikiliza anaweza kupata kwamba mtoto wako hakupokea FAPE kama tu ukiukaji kwa utaratibu:

1. Kuliingiliana na haki ya mtoto wako ya elimu ya bure inayofaa umma (FAPE);
2. Kuliingiliana vilivyo na nafasi yako ya kuhusika katika mchakato wa kufanya uamuzi kuhusu utoaji wa elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
3. Kulisababisha *mtoto wako kupungukiwa kwa manufaa ya kielimu.*

Ibara ya uundaji

Hamna toleo lolote lililofafanuliwa hapo juu linaweza kutafsiriwa kama kumzuia afisa wa kusikiliza kuamuru wilaya ya shule kufuata mahitaji kwenye sehemu ya kuhifadhi utaratibu ya maagizo ya Jimbo chini ya Sehemu B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536).

Ombi la kando la kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa

Hakuna chochote kwenye sehemu ya kuhifadhi utaratibu wa maagizo ya Jimbo chini ya Sehemu B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536) inaweza kutafsiriwa kama inakuzuia

wewe kuwasilisha malalamiko ya kando ya mchakato unaotazamiwa juu ya suala kando na malalamiko ya mchakato unaotazamiwa ambao tayari umewasilishwa.

Matokeo na uamuzi wa jopo la ushauri na umma kwa ujumla

Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule, (yeyote aliyewajibika kwa kusikilizwa kwako) baada ya kufuta habari zozote za kibinafsi zinazoweza kutambuliwa, lazima:

1. Atoe matokeo na maamuzi ya kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa au akate rufaa kwa jobo la ushauri wa elimu maalum ya Serikali; **na**
2. Afanye matokeo hayo na maamuzi hayo yapatikane kwa umma.

RUFAA

KUKAMILIKA KWA UAMUZI; KUKATA RUFAA; UHAKIKI ADILIFU

34 CFR §300.514

Kukamilika kwa uamuzi wa kusikilizwa

Uamuzi unaofanywa wakati wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa (pamoja na kusikilizwa kunakohusiana na utaratibu wa kufunza nidhamu) ni wa mwisho, isipokuwa kama chama chochote kinachohusika katika kusikilizwa (wewe au wilaya ya shule) kikate rufaa juu ya uamuzi huo kwa kuleta hatua ya madai, kama ilivyofafanuliwa hapo [chini] *chini ya kichwa* **Matendo ya Kiraia, Ikijumuisha Muda wa Wakati Imbayo ni ya Kuwasilisha Matendo Hayo.**

MUDA MAALUM NA URAHISI WA KUSIKILIZWA NA UHAKIKI

34 CFR §300.515

Chombo cha Elimu cha Serikali lazima kihakishe kwamba isipite siku 45 za kalenda baada ya kuisha kwa siku 30 za kalenda za kipindi cha mkutano wa suluhisho **au**, kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa-kidogo cha ***Marekebisho ya siku 30 za kalenda za kipindi cha suluhisho***, isipite siku 45 za kalenda baada ya kuisha kwa kipindi cha muda uliorekebishwa:

1. Uamuzi wa mwisho ufikiwe kwa kusikilizwa, **na**
2. Nakala ya uamuzi itumwe kwa kila chama.

Afisa wa kusikiliza anaweza kuongeza muda maalum zaidi ya kipindi cha muda wa siku 45 za kalenda hapo juu chama chochote kikiomba.

Kila kusikilizwa lazima kufanywe kwa wakati na mahali ambapo ni rahisi kwako na kwa mtoto wako.

HATUA ZA MADAI, PAMOJA NA KIPINDI CHA MUDA AMBAO UNAWEZA KUWASILISHA HATUA HIZO

34 CFR §300.516

Kwa ujumla

Chama chochote (wewe au wilaya ya shule) kisicho kubali matokeo na uamuzi wa kusikilizwa kwa mchakato unao tazamiwa (pamoja na kusikilizwa kunako husiana na utaratibu wa kufunza nidhamu) kinahaki ya kuleta hatua ya madai inayo husiana na hoja ambayo ilikuwa suala la kusikilizwa kwa mchakato unao tazamiwa. Hatua hiyo inaweza kuletwa kwa korti ya Serikali yenye mamlaka ya kisheria (korti ya Serikali ambayo ina mamlaka ya kusikiliza kesi ya aina hii) au katika korti ya wilaya ya Merikani bila kuzingatia ukubwa wa mzozo.

Kizuizi cha muda

Chama ambacho kinaleta hatua hiyo (wewe au wilaya ya shule) kitakuwa na siku 45 za kalenda kuanzia tarehe ya uamuzi wa afisa wa kusikiliza wa kuwasilisha hatua ya madai.

Utaratibu zaidi

Katika hatua yoyote ya madai, korti:

1. Hupokea rekodi za msimamizi wa kesi;
2. Husikia ushahidi zaidi wewe ukiomba au wilaya ya shule ikiomba; **na**
3. Huweka uamuzi wake kwa kuwepo kwa ushahidi na hupeana msaada ambao korti huonelea unafaa.

Chini ya hali mwafaka, usaidizi wa mahakama unaweza kujumuisha kurudishiwa masomo ya ziada kwa shule za kibinafsi na huduma ya kufidiwa ya elimu.

Mamlaka ya kisheria ya korti za wilaya

Korti za wilaya za Marekani zina mamlaka ya kutoa uamuzi wa hatua zilizoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA bila kuzingatia ukubwa wa mzozo.

Sheria ya uundaji

Hakuna kitu chochote katika Sehemu B ya IDEA kinachopinga au kuzuia haki, utaratibu na marekebisho yanayopatikana chini ya Katiba ya Marekani, Sheria ya 1990 ya Waamerika walemavu, Kichwa cha V cha sheria ya Urekebishaji ya 1973 (Sehemu ya 504), au sheria zingine za Jimbo zinazolinda haki za watoto walemavu, isipokuwa kama kabla ya kuwasilishwa kwa hatua ya madai chini ya sheria hizi ukitafuta msaada ambao unapatikana pia chini ya Sehemu B ya IDEA, utaratibu wa mchakato unaotazamiwa uliofafanuliwa hapo juu lazima utumiwe kabisa kama vile ingelivyotumiwa kama inavyohitajika ikiwa chama hicho kingewasilisha hatua hiyo chini ya Sehemu B ya IDEA. Hii inamaanisha kwamba unaweza kuwa na marekebisho yanayopatikana chini ya sheria zingine ambazo zinapitana na zile zinazopatikana chini ya IDEA, ili upate usaidizi chini ya sheria hizo, lakini kwa ujumla, lazima kwanza utumie marekebisho ya msimamizi yanayopatikana chini ya IDEA (k.v., malalamiko ya mchakato unaotazamiwa, mkutano wa suluhisho, na utaratibu wa kusikilizwa kwa mchakato adilifu unaotazamiwa) kabla ya kwenda moja kwa moja kortini.

KUWEKWA KWA MTOTO WAKATI WA MCHAKATO UNAOTAZAMIWA MALALAMISHI NA KUSIKIZWA KWA KESI KUKIWA BADO KUNAGOJEWA

34 CFR §300.518

Bali na ilivyo tolewa hapo chini ya kichwa ***UTARATIBU WAKATI UNAPO WAADHIBU WATOTO WALEMAVU,*** mara tu mchakato wa malalamishi unaotazamiwa unatumwa kwa mhusika mwingine wakati wa kutayarisha suluhusho, na wakati wa kungojea uamuzi wowote wa uadilifu wa mchakato unaotazamiwa kusikilizwa au utaratibu wa mahakama, ila tu wewe na Taifa auwilaya ya shule wanakubaliana vinginevyo , mtoto wako ni lazima abaki katika mahali alipo wekwa pa elimu.

Ikiwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa itahusisha ombi la kwanza la kusajiliwa katika shule ya umma, mtoto wako, na ruhusa yako, ni lazima awekwe katika kipindi cha shule ya kawaida ya umma hadi mwisho wa utaratibu hiyo yote.

Ikiwa malalamiko ya mchakato unaotazamiwa itahusisha huduma za kwanza chini ya Sehemu ya B ya IDEA kwa mtoto ambaye ana mabadiliko kutoka kuhudumiwa chini ya Sehemu C ya IDEA hadi kwa Sehemu B ya IDEA na haifai kwa huduma za Sehemu ya C kwa sababu mtoto amefikisha miaka mitatu, shule ya wilaya haitajiki kutoa huduma za Sehemu ya C ambayo mtoto amekuwa akipokea. Ikiwa mtoto atapatikana anafaa chini ya Sehemu ya B ya IDEA na umruhusu mtoto apokee elimu maalum na huduma ziambatanazo kwa mara ya kwanza, kasha, wakati wa kungoja matokeo ya utaratibu, wilaya ya shule ni lazima itoe elimu hizo maalum na huduma ziambatanazo ambazo hazileti mabishano (zile ambazo wewe na shule ya wilaya nyinyi wote mmekubaliana).

Ikiwa afisa wa kusilikiza ako kwa mchakato wa kusikilizwa unaotazamiwa inayo endeshwa na Ajenti wa Elimu ya Taifa ana kubaliana nawe kuwa mabadiliko ya uhaliwishaji ni mwafaka, uhaliwishaji huo ni lazima ushughulikiwe kama uhaliwishaji wa elimu ya mtoto wako wa hivi punde ambapo mtoto wako atabaki wakati akingojea uamuzi wowote adilifu wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa au utaratibu wa mahakama.

ADA YA WAKILI

34 CFR §300.517

Kwa ujumla

Katika hatua yoyote au kesi iliyoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, ukiendelea, korti, kwa kupendelea kwake, inaweza kutuza ada ya wakili kama sehemu ya gharama kwako.

Katika hatua yoyote au kesi iliyoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, korti, kwa kupendelea kwake, inaweza kutuza ada ya wakili kama sehemu ya gharama kwa Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule, ilipwe na wakili wako, ikiwa wakili huyo: (a) amewasilisha malalamiko au kesi ya korti ambayo korti inapata ni hafifu, isiyoeleweka, au isio na msingi ; **au** (b) ameendelea kuenda mahakamani baada ya madai kuwa hafifu, yasiyoeleweka, au yasio na msingi; **au**

Katika hatua yoyote au kesi iliyoletwa chini ya Sehemu B ya Idea, korti, kwa kupendelea kwake, inaweza kutuza ada ya wakili kama sehemu ya gharama kwa Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule, ilipwe na wakili wako, ikiwa ombi lako la kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa au kesi ya baadaye ya korti ililetwa kwa sababu zisizostahili, kama vile kunyanyasa, kusababisha upotezaji wa wakati, au kuongeza gharama ya hatua hiyo au kesi hiyo.

Tuzo la ada

Korti hutuza ada ya wakili kama inavyofuata:

1. Ada lazima msingi wake iwe viwango vilivyo kwenye jamii ambayo hatua hiyo au utaratibu ambao ulianza kwa aina na uzuri wa huduma zilizotolewa. Hakuna bonasi au kichanganyiko kinachoweza kutumiwa katika kuhesabu ada itakayotuzwa.
2. Ada haiwezi kutuzwa na gharama zinazolingana haziwezi kurudishwa katika hatua au kesi yoyote chini ya Sehemu B ya IDEA ya huduma zilizotekelezwa baada ya toleo uliloandikiwa la maafikiano ikiwa:
   a. Toleo hilo limefanywa kati ya muda uliofafanuliwa na Sheria ya 68 ya Sheria za Jimbo za Utaratibu wa Madai au, katika hali ya kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa au uhakiki wa kiwango cha Serikali, wakati wowote zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya kesi kuanza;
   b. Toleo hilo halikubaliwi kati ya siku 10 za kalenda; **na**
   c. Korti au afisa msimamizi wa kusikiliza akipata kwamba usaidizi ambao ulipata mwishowe haukufai zaidi ya toleo lile lingine la maafikiano.

   Licha ya vizuizi hivi, tuzo la ada ya wakili na gharama zinazohusiana zinaweza kufanywa kwako ikiwa utaendelea na kama ulihesabiwa haki kwa kukataa toleo la maafikiano.
3. Ada inayohusiana na mkutano wowote wa Kikundi cha elimu ya kibinafsi (IEP) haitatuzwa isipokuwa mkutano huo ufanywe kama matokeo ya msimamizi wa kesi au hatua ya korti.
   Mkutano wa suluhisho, kama ilivyofanuliwa chini ya kichwa cha Utaratibu wa suluhisho, hauchukuliwi kama mkutano ulioitwa kama matokeo ya kusikilizwa kwa msimamizi au hatua ya korti, na pia haichukuliwi kama kusikilizwa kwa msimamizi au hatua ya korti kwa madhumuni ya toleo hizi za ada ya wakili.

Korti hupunguza, kama inavyostahili, kiwango cha ada ya wakili inayotuzwa chini ya Sehemu B ya IDEA, kama korti itapata kwamba:

1. Wewe, au wakili wako, wakati wa mkondo wa hatua au kesi, mlichelewesha suluhisho la mwisho la mzozo;
2. Kiwango cha ada ya wakili kiilichoidhinishwa kituzwe kilipita kiwango cha kila saa kiliopo katika jamii kwa huduma sawa ya mawakili wenye ustadi, sifa na ujuzi huo mmoja.
3. Muda uliochukuliwa na huduma za kisheria zilizotolewa zilipita kiasi kulingana na hali ya hatua au kesi; **au**
4. Wakili anayekuwakilisha hakupatia wilaya ya shule habari zinazofaa katika ilani ya ombi la mchakato unaotazamiwa kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa.***

Walakini, korti haiwezi kupunguza ada ikiwa korti itapata kwamba Serikali au wilaya ya shule ilichelewesha suluhisho la mwisho la hatua au kesi au kulikuwa na ukeukaji chini ya utoaji wa kuhifadhi utaratibu ya Sehemu B ya IDEA.

UTARATIBU UNAOFUATWA WAKATI WA KUADHIBU WATOTO WENYE ULEMAVU

MAMLAKA YA MTUMISHI WA SHULE

34 CFR §300.530

Uamuzi wa kesi kwa kesi

Mtumishi wa shule anaweza kuzingatia hali yoyote ya kipekee kwa misingi ya kesi kwa kesi, wakati unapoamua kubadilisha mahali, iliyofanywa kulingana na mahitaji yanayofuata yanayohusiana na tabia, inamfaa mtoto mlemavu ambaye anakeuka kanuni ya shule ya mwenendo wa mwanafunzi.

Kwa ujumla

Kwa kadiri kwamba pia wanachukua hatua kama hiyo kwa watoto wasio na ulemavu, mtumishi wa shule anaweza, kwa **siku zisizopita 10 za shule** zikifuatana, kumwondoa mtoto mlemavu ambaye anakeuka kanuni za mienendo ya wanafunzi kutoka mahali pake pa sasa hadi kwa mpangilio mwingine wa elimu ya muda unaofaa (mpangilio mwingine, au kusimamishwa. Mtumishi wa shule pia anaweza kuongeza uhamisho zaidi kwa mtoto **kwa siku zisizopita 10 za shule** zikifuatana katika mwaka huo mmoja wa shule kwa matukio tofauti za makosa, maadamu uhamisho huo haujumuishi mabadiliko ya mahali (angalia hapo chini ***Mabadiliko ya Mahali kwa sababu ya Uhamisho wa Kinidhamu*** kwa ajili ya ufafanuzi).

Mara tu mtoto mlemavu akihamishwa kutoka kwa mahali pake pa sasa kwa jumla ya **siku 10 za shule** katika mwaka mmoja wa shule, wilaya ya shule lazima, wakati wa siku za uhamisho zinazofuata katika mwaka huo wa shule, itoe huduma kama inavyotakikana hapo chini, chini ya kichwa-kidogo cha **Huduma.**

Mamlaka ya ziada

Ikiwa tabia iliyokeuka kanuni za mienendo ya wanafunzi haikuwa onyesho la ulemavu wa mtoto (angalia hapo chini ***Uamuzi wa onyesho***) na mabadiliko ya kinidhamu ya mahali inaweza kupita **siku 10 za shule** zikifuatana, mtumishi wa shule anaweza kutumia utaratibu wa nidhamu kwa mtoto huyo mlemavu kwa njia sawa na muda sawa kama ingelivyokuwa kwa watoto wasio na ulemavu, isipokuwa shule hiyo lazima itoe huduma kwa mtoto huyo kama ilivyofafanuliwa hapo chini, chini ya ***Huduma.*** Kikundi cha mtoto cha EIP huamua mpangilio mwingine wa elimu ya muda kwa huduma kama hiyo.

Huduma

Huduma ambazo lazima zitolewe kwa mtoto mlemavu ambaye amehamishwa kutoka mahali pake pa sasa zinaweza kutolewa katika mpangilio mwingine wa elimu ya muda.

Wilaya ya shule inahitajika tu kutoa huduma kwa mtoto mlemavu ambaye amehamishwa kutoka mahali pake pa sasa kwa **siku 10 za shule au chini** katika mwaka huo wa shule, ikiwa hutoa huduma kwa mtoto asiye na ulemavu ambaye amehamishwa vivyo hivyo.

Mtoto mlemavu ambaye amehamishwa kutoka mahali pake pa sasa kwa zaidi ya **siku 10 za shule** na tabia si dhahiri kwa ulemavu wa mtoto (tazama kichwa kidogo cha **azimio la Dhahiri**)

au ambaye ametolewa chini ya matukio maalum (tazama kichwa kidogo. ***Matukio maalum***) lazima:

1. Aendelee kupokea huduma za kielimu (wana elimu mwafaka ya umma ya bure) , ili kumwezesha mtoto aendelee kuhusika katika mtalaa wa elimu ya jumla, ijapokuwa katika mpangilio mwingine (ambayo yaweza kuwa mpangilio mbadala wa elimu wa muda) , na kuendelea kuwadia kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto; **na**
2. Apokee, kama inavyotakikana, uchunguzi unaotumika wa kitabia, na huduma za uingiliaji tabia na urekebishaji, ambazo zimeundwa ili kushughulikia ukeukaji wa tabia ili isifanyike tena.

Baada ya mtoto mlemavu kuhamishwa kutoka mahali pake pa sasa kwa **siku 10 za shule** katika mwaka huo mmoja wa shule, na **ikiwa** uhamisho wa sasa ni wa siku **10 za shule** zikifuatana au chini na ikiwa uhamisho huo sio mabadiliko ya mahali (angalia ufafanuzi hapo chini), **basi** mtumishi wa shule, kwa kushauriana na mmoja wa waalimu wa mtoto, anaweza kuamua umbali ambao huduma zitahitajika ili kumwezesha mtoto kuendelea kuhusika katika mtalaa wa elimu ya jumla, ijapokuwa katika mpangilio mwingine, na kuendelea kuwadia kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

Ikiwa uhamisho ni mabadaliko ya mahali (angalia kichwa, ***Mabadiliko ya Mahala kwa ajili ya Uondoaji wa Kinidhamu***), Kikundi cha mtoto cha IEP kitaamua huduma zinazofaaa ili kumwezesha mtoto kuendelea kuhusika katika mtalaa wa elimu ya jumla, ijapokuwa katika mpangilio mwingine (*ambayo yaweza kuwa mpangilio mbadala wa elimu wa muda)*, na kuendelea kuwadia kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

Uamuzi wa onyesho

Kati ya **siku 10 za shule** za uamuzi wowote wa kubadilisha mahali pa mtoto mlemavu kwa sababu ya ukeukaji wa kanuni za mienendo ya wanafunzi (isipokuwa uhamisho ambao ni wa **siku 10 za shule** zikifuatana au chini na wala sio mabadiliko ya mahali), wilaya ya shule, wewe, na wanachama wengine wanaofaa wa Kikundi cha IEP (kama ilivyoamuliwa na wewe na wilaya ya shule) lazima ahakiki habari zote zinazofaa katika faili ya mwanafunzi, pamoja na IEP ya mtoto, uchunguzi wowote wa mwalimu, na habari zozote zinazofaa zilizotolewa na wazazi ili waamue:

1. Kama mwenendo unaoshughulikiwa ulisababishwa, au ulikuwa na uhusiano dhabiti na wa moja kwa na ulemavu wa mtoto; **au**
2. Kama mwenendo unaoshughulikiwa ulikuwa ni matokeo ya moja kwa moja ya wilaya ya shule kukosa kutekeleza IEP ya mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na wanachama wanaofaa wa Kikundi cha mtoto cha IEP wakiamua kwamba hali hizo zote zilifikiwa, mwenendo huo lazima uamuliwe kuwa ni onyesho la ulemavu wa mtoto.

Ikiwa wilaya shule, wewe, na wanachama wanaofaa wa Kikundi cha mtoto cha IEP wakiamua kwamba mwenendo unaoshughulikiwa ulikuwa matokeo ya moja kwa moja ya shule kukosa kutekeleza IEP, wilaya ya shule lazima ichukue hatua ya moja kwa moja ya kurekebisha upungufu huo.

Uamuzi wa kwamba tabia ilikuwa onyesho la ulemavu wa mtoto

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na wanachama wanaofaa wa Kikundi cha IEP wakiamua kwamba mwenendo huo ulikuwa onyesho la ulemavu wa mtoto, Kikundi cha IEP aidha lazima:

1. Kifanye uchunguzi unaotumika wa kitabia, isipokuwa wilaya ya shule ilikuwa imefanya uchunguzo unaotumika wa kitabia kabla ya tabia ambayo ilisababisha mabadiliko yaliyofanywa ya mahali, na kutekeleza mpango wa kuingilia tabia ya mtoto; **au**
2. Ikiwa mpango wa uingiliaji wa kitabia tayari umeanzishwa, kihakiki mpango wa kuingilia tabia, na kuirekebisha kama inavyotakikana, ili ishughulikie tabia hiyo.

Isipokuwa kama ilivyofafanuliwa hapo chini, chini ya kichwa-kidogo cha ***Hali maalum***, wilaya ya shule lazima imrudishe mtoto huyo mahali ambapo mtoto huyo alihamishwa, isipokuwa wewe na wilaya ikubali kubadilisha mahali hapo kama sehemu ya kurekebisha mpango wa kuingilia tabia.

Hali maalum

Iwe tabia ilikuwa onyesho la ulemavu wa mtoto au hapana, mtumishi wa shule anaweza kumwamisha mwanafunzi hadi kwa mpangilio mwingine wa elimu ya muda (inayoamuliwa na Kikundi cha mtoto cha IEP) hadi siku 45 za shule, ikiwa mtoto:

1. Anabeba silaha shuleni au ana silaha shuleni (angalia ufafanuzi hapo chini), kwa majengo ya shule, au kwa hafla ya shule chini ya mamlaka ya kisheria ya Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule;
2. Kwa kujua anatumia au ana madawa yasio halali (angalia ufafanuzi hapo chini), au anauza au anaomba mauzo ya kitu kinachodhibitiwa, (angalia ufafanuzi hapo chini), akiwa shuleni, kwa majengo ya shule, au kwa hafla ya shule chini ya mamlaka ya kisheria ya Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule; **au**
3. Amemuumiza mtu mwingine vibaya sana kimwili (angalia ufafanuzi hapo chini), akiwa shuleni, kwa majengo ya shule, au kwa hafla ya shule chini ya mamlaka ya kisheria ya Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule.

Ufafanuzi

Kitu kinachodhibitiwa inamaanisha dawa au kitu kingine kinachotambuliwa chini ya ratiba I, II, III, IV, au V katika sehemu ya 202 (c) ya Sheria ya Vitu Vinavyodhibitiwa (21 U.S.C. 812 (c)).

Dawa isiyo halali inamaanisha kitu kinachodhibitiwa; lakini haijumuishi kitu kinachodhibitiwa ambacho kinamilikiwa kihalali au kutumiwa chini ya usimamizi wa mtaalam wa kimatibatu aliyeidhinishwa au ambayo inamilikiwa kihalali au kutumiwa chini ya utawala mwingine chini ya Sheria hiyo au chini ya utoaji mwingine wowote wa Sheria ya Serikali.

Kuumizwa vibaya sana kimwili ina umaana uliyopewa neno la "kuumizwa vibaya sana kimwili" chini ya aya ya (3) ya sehemu ndogo ya (h) ya sehemu ya 1365 ya kichwa cha 18, Kanuni za Marekani.

Silaha ina umaana uliyopewa neno la “silaha hatari” chini ya aya ya (2) ya sehemu ndogo ya kwanza ya (g) ya sehemu ya 930 ya kichwa cha 18, Kanuni za Marekani.

Taarifa

Tarehe ile ambayo uamuzi unafanywa wa kufanya uhamisho ambao ni mabadiliko ya sehemu ya mtoto kwa sababu ya ukeukaji wa kanuni za mienendo ya wanafunzi, wilaya ya shule lazima ikujulishe wewe juu ya uamuzi huo, na wewe ilani ya kuhifadhi utaratibu.

MABADILIKO YA MAHALI KWA SABABU YA UHAMISHO WA KINIDHAMU

34 CFR §300.536

Kuhamishwa kwa mtoto wako mlemavu kutoka mahali pake pa sasa pa elimu ni **mabadiliko ya mahali** ikiwa:

1. Uhamisho huo ni wa zaidi ya siku 10 za shule zikifuatana; **au**
2. Mtoto wako amepitia misururu ya uhamisho ambayo yanajumuisha mtindo kwa sababu:
   a. Misururu hiyo ya uhamisho kwa ujumla ni zaidi ya siku 10 za shule kwa mwaka wa shule;
   b. Tabia ya mtoto wako ni sawa kabisa na tabia ya mtoto huyo katika matukio ya hapo awali ambayo yalisababisha misururu hiyo ya uhamisho;
   c. Kama vile mambo ya ziada kama urefu wa kila uhamisho, ujumla wa kiwango cha wakati ambao mtoto huyo amehamishwa, na kukaribiana kwa uhamisho na ule mwingine.

Iwe au isiwe mtindo wa uhamisho unaojumuisha mabadiliko ya mahali yanaamuliwa kwa misingi ya kesi kwa kesi na wilaya ya shule na, kama itapingwa, inaweza kuhakikiwa kupitia mchakato unaotazamiwa na kesi ya kisheria.

UAMUZI WA MPANGILIO

34 CFR §300.531

Kikundi cha mpango wa kibinafsi wa elimu (IEP) inaamua mpangilio mwingine wa elimu ya muda ya uhamisho ambayo ni **mabadiliko ya mahali**, na uhamisho chini ya vichwa vidogovha ***Mamlaka ya ziada*** na ***Hali maalum***.

KUKATA RUFAA

34 CFR §300.532

Kwa ujumla

Unaweza kukata rufaa ya malalamiko ya mchakato unaotazamiwa (angalia ***Utaratibu wa Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa***) ili aombe kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa ikiwa yeye hakubaliani na:

1. Uamuzi wowote unaohusiana na mahali uliofanywa chini ya utoaji wa tabia; **au**
2. uamuzi wa onyesho uliofafanuliwa hapo juu.

Wilaya ya shule inaweza kuwasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa (angalia hapo juu) ili aombe kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa ikiwa anaamini kwamba kutunza mahali pa sasa pa mtoto kunaweza kusababisha kuumia kwa mtoto au kuumia kwa wengine.

Mamlaka ya afisa wa kusikiliza

Afisa wa kusikiliza ambaye anafikia mahitaji yaliyofafanuliwa chini ya kichwa-kidogo cha ***Afisa mwadilifu wa kusikiliza*** lazima atekeleze kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa na afanye uamuzi. Afisa wa kisikiliza anaweza:

1. Mrudishe mtoto wako mlemavu mahali ambapo mtoto wako alihamishwa ikiwa afisa wa kusikiliza ataamua kwamba uhamisho huo ulikuwa ukeukaji wa mahitaji yaliyofafanuliwa chini ya kichwa cha ***Mamlaka ya mtumishi wa shule***, au kwamba tabia ya mtoto wako ilikuwa onyesho la ulemavu wa mtoto wako; **au**
2. Kuamuru mabadiliko ya mahali pa mtoto wako mlemavu hadi kwa mpangilio mwingine wa elimu ya muda isiyozidi siku 45 za shule ikiwa afisa wa kusikiliza akiamua kwamba kutunza mahali pa sasa pa mtoto wako inaweza kusababisha kuumia kwa mtoto wako au kuumia kwa wengine.

Utaratibu huu wa kusikilizwa unaweza kurudiwa, ikiwa wilaya ya shule inaamini kwamba kumrudisha mtoto wako mahali pake pa asili inaweza kusababisa kuumia kwa mtoto wako au kuumia kwa wengine.

Wakati wowote wewe au wilaya ya shule inapowasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa ya kuomba kusikilizwa kama huko, kusikilizwa lazima kufanyike ambako kunafikia mahitaji yaliyofafanuliwa chini ya vichwa vya ***Utaratibu wa Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa, Kusikilizwa kwa Malalamiko ya Mchakato Unaotazamiwa***, isipokuwa kama ifwatavyo:

1. Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule lazima ifanye mipango ya kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa ulioharakishwa, ambao lazima ufanywe kati ya siku **20** za shule kwanzia tarehe ya maombi ya kusikilizwa na lazima itoe matokeo ya uamuzi kati ya siku **10** za shule baada ya kusikilizwa.
2. Isipokuwa wewe na wilaya ya shule ikubali kuondoa mkutano kwa kuandika, au ikubali kutumia upatanisho, mkutano wa suluhisho lazima ufanyike kati ya siku **saba** za kalenda baada ya kupokea ilani ya malalamiko ya mchakato unaotazamiwa. Kusikilizwa kunaweza kuendelea isipokuwa suala hilo liwe limetatuliwa hadi vyama vyote viridhike kati ya siku **15** za kalenda baada ya kupokea malalamiko ya mchakato unaotazamiwa.
3. Serikali inaweza kuanzisha sheria tofauti za utaratibu ili kuharakisha kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa zaidi ya vile ilivyoanzisha kwa kusikilizwa kwingine kwa mchakato unaotazamiwa, lakini isipokuwa kwa muda maalum, sheria zile ambazo lazima zifuatane na sheria ndani ya hati hii kuhusiana na kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa.

Wewe au wilaya ya shule mnaweza kukata rufaa uamuzi wa kusikilizwa kwa mchakato unaotazamiwa ulioharakishwa kwa njia sawa na kama vile kiwezavyo kwa kusikilizwa kwingine kwa mchakato unaotazamiwa (angalia ***Kukata rufaa***, hapo juu).

MAHALI WAKATI WA KUKATA RUFAA

34 CFR §300.533

Kama ilivyofafanuliwa hapo juu, wakati wewe au wilaya ya shule inapowasilisha malalamiko ya mchakato unaotazamiwa unaohusiana na masuala ya kinidhamu, mtoto wako ni lazima abakie kwa mpangilio mwingine wa elimu ya muda akisubiri uamuzi wa afisa wa kusikiliza, au hadi kuisha kwa kipindi cha muda wa kuhamishwa kama ilivyotolewa na kufafanuliwa chini ya kichwa cha ***Mamlaka ya Mtumishi wa Shule,*** yoyote itakayofanyika kwanza (isipokuwa wewe na Chombo cha Elimu cha Serikali au wilaya ya shule ikubali)

ULINZI KWA WATOTO AMBAO HAWAJASTAHIKI ELIMU MAALUM NA HUDUMA ZINAZOLINGANA

34 CFR §300.534

Kwa ujumla

Ikiwa mtoto wako hajaamuliwa kwamba anastahiki elimu maalum na huduma zinazolingana na akeuke kanuzi za mienendo ya wanafunzi, lakini wilaya ya shule iwe ilijua (kama ilivyoamuliwa hapo chini) kabla ya tabia hiyo ambayo ilisababisha hatua iliyofanyika ya kinidhamu, ya kwamba mtoto wako alikuwa mtoto mlemavu, basi mtoto wako anaweza kudai ulinzi wowote uliofafanuliwa katika ilani hii.

Misingi ya ufahamu kwa masuala ya kinidhamu

Wilaya ya shule itaonekane kuwa ilijua kwamba mtoto wako ni mtoto mlemavu ikiwa, kabla ya tabia ambayo ilisababisha hatua iliyofanyika ya kinidhamu:

1. Wewe ulionyesha shaka kwa kuandika kwa mtumishi mwangalizi au msimamizi wa chombo kifaacho, au kwa mwalimu wa mtoto wako anahitaji elimu maalum na huduma ziambatanazo;
2. Wewe uliomba tathmini inayohusiana na kustahiki elimu maalum na huduma zinazolingana chini ya Sehemu B ya IDEA; **au**
3. Mwalimu wa mtoto wako, au mtumishi mwingine wa wilaya ya shule alionyesha shaka maalum kuhusu mtindo wa kitabia ulionyeshwa na mtoto huyo moja kwa moja kwa mkurugenzi wa wilaya ya shule ya elimu maalum au kwa mtumishi mwingine mwangalizi wa wilaya ya shule.

Kinzano

Wilaya ya shule haitaonekana kuwa ilijua ikiwa:

1. hajaruhusu tathmini ya mtoto au alikataa huduma ya elimu maalum; **au**
2. Mtoto wako ametathminiwa na akaamuliwa kuwa si mtoto mlemavu chini ya Sehemu B ya IDEA.

Hali zinazotumika kama hakuna misingi ya ufahamu

Ikiwa kabla ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtoto wako, wilaya ya shule haikuwa ikijua kwamba mtoto wako ni mtoto mlemavu, kama ilivyofafanuliwa hapo juu chini ya kichwa-kidogo cha ***Misingi ya ufahamu kwa masuala ya kinidhamu*** na ***Kinzano***, mtoto huyo

anaweza kupitia hatua za kinidhamu ambazo zinatumika kwa watoto wasio walemavu ambao hujihusisha na tabia kama hizo.

Walakini, kama ombi litafanywa la tathmini ya mtoto wako wakati wa kipindi cha muda ambao mtoto wako anapitia hatua za kinidhamu, tathmini hiyo lazima itekelezwe kwa njia ya upesi.

Hadi tathmini hiyo ikamilike, mtoto wako hubakia katika mahali pa elimu palipoamuliwa na utawala wa shule, ambayo inaweza kujumuisha kusimamishwa au kufukuzwa bila huduma za kielimu.

Ikiwa mtoto wako ataamuliwa kuwa mtoto mlemavu, tukizingatia habari kutoka kwa tathmini iliyofanywa na wilaya ya shule, na habari zilizotolewa na wewe, wilaya ya shule lazima itoe elimu maalum na huduma zinazolingana kulingana na Sehemu B ya IDEA, pamoja na mahitaji ya kinidhamu yaliyofafanuliwa hapo juu.

REJELEO LA HATUA YA WATEKELEZA SHERIA NA WATAWALA WA KIMAHAKAMA

34 CFR §300.535

Sehemu B ya IDEA:

1. Haizuilii chombo kutokana na kuripoti uhalifu uliofanywa na mtoto mlemavu kwa utawala unaofaa; **au**
2. Haiwazuilii watekelezaji sheria wa Serikali na watawala wa kimahakama kutokana na kutekeleza uwajibikaji wao kuhusu kutumiwa kwa Sheria ya Jimbo na Serikali juu ya uhalifu uliofanywa na mtoto mlemavu.

Upitishaji wa rekodi

Wilaya ya shule ikiripoti uhalifu uliofanywa na mtoto mlemavu, wilaya ya shule:

1. Lazima ihakikishe kwamba nakala za rekodi za kinidhamu na elimu maalum ya mtoto zimepitishwa ili zizingatiwe na utawala ambao chombo hicho kiliripoti uhalifu huo; **na**
2. Inaweza kupitisha nakala za rekodi za kinidhamu na elimu maalum ya mtoto kwa kadiri iliyoidhinishwa na Sheria ya Siri na Haki ya Elimu ya Jamii (FERPA).

MATAKWA YA MAHALI PA TAIFA MOJA YA WAZAZI WA WATOTO WALIO KATIKA SHULE ZA KIBINAFSI KWA GHARAMA YA UMMA

KWA UJUMLA

34 CFR §300.148

Sehemu B ya IDEA haihitaji wilaya ya shule ilipie gharama ya elimu, pamoja na elimu maalum na huduma zinazolingana, za mtoto wako mlemavu aliye katika shule ya kibinafsi au jengo ikiwa wilaya ya shule ilifanya elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) ipatikane

kwa mtoto wako na wewe ukachagua kumweka mtoto wako katika shule ya kibinafsi au jengo. Walakini, wilaya ya shule ambayo shule ya kibinafsi ipo lazima imjumuishe mtoto wako kati ya watu ambao mahitaji yao yameshughulikiwa chini ya utoaji wa Sehemu B kuhusu watoto ambao wamewekwa na wazazi wao katika shule ya kibinafsi chini ya 34 CFR 300.131 hadi 300.144.

Kurudishiwa gharama ya kuwekwa katika shule ya kibinafsi

Ikiwa mtoto wako hapo awali alipokea elimu maalum na huduma zinazolingana chini ya utawala wa wilaya ya shule, na uchague kumwandikisha mtoto wako katika shule ya mapema ya kibinafsi, shule ya msingi, au shule ya upili bila ruhusa au kuelekezwa na wilaya ya shule, korti au afisa wa kusikiliza anaweza kuhitaji chombo hicho kikurudishie gharama ya kuandikishwa huko ikiwa korti au afisa wa kusikiliza atapata kwamba chombo hicho hakikufanya elimu ya bure inayofaa umma (FAPE) ipatikane kwa mtoto wako kwa wakati unaofaa kabla ya kuandikishwa huko na kwamba mahali hapo pa kibinafsi panafaa. Afisa wa kusikiliza au korti inaweza kupata kwamba mahali hapo panafaa, hata kama mahali hapo hapafikii viwango vya Serikali ambavyo vinatumika kwa elimu iliyotolewa na Chombo cha Elimu cha Serikali na wilaya ya shule.

Kizuizi cha kurudishiwa gharama

Gharama itakayorudishwa iliyofafanuliwa katika aya iliyo hapo juu inaweza kupunguzwa au kukataliwa:

1. Ikiwa: (a) Katika mkutano wa hivi karibuni wa mpango wa elimu ya kibinafsi (IEP) ambayo ulihudhuria kabla ya mtoto wako kuhamishwa kutoka kwa shule ya umma, haukujulisha kikundi cha IEP kwamba ulikuwa ukikataa mahali ambapo palipendekezwa na wilaya ya shule ili itoe FAPE kwa mtoto wako, pamoja na kusema hoja yako na lengo lako la kumwandikisha mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama ya umma; au (b) Kabla ya siku 10 za biashara kabla ya mtoto wako kuhamishwa kutoka kwa shule ya umma (pamoja na siku zozote za mapumziko ambazo zinatokea wakati wa siku za biashara), haukupeana ilani iliyoandikwa kwa wilaya ya shule juu ya habari hizo;
2. Ikiwa, kabla ya mtoto wako kuhamishwa kutoka kwa shule ya umma, wilaya ya shule ilikupa ilani iliyoandikwa mapema, juu ya lengo lake la kumtathmini mtoto wako (pamoja na taarifa ya madhumuni ya tathmini ambayo ilifaa na iliyokuwa ya busara), lakini haukufanya mtoto apatikane kwa ajili ya tathmini hiyo; **au**
3. Baada ya matokeo ya korti ya kuwa hatua zako hazikuwa za busara.

Walakini, gharama itakayorudishwa:

1. Lazima isipunguzwe wala kunyimwa kwa kukosa kutoa ilani ikiwa: (a) Shule ilikuzuia usitoe ilani hiyo; (b) Haukupokea ilani ya uwajibikaji wako wa kutoa ilani hiyo iliyofafanuliwa hapo juu; au (c) Kufuata mahitaji yaliyo hapo juu yangesababisha madhara ya kimwili kwa mtoto wako; **na**
2. Korti ikipendelea au afisa wa kusikiliza akipendelea, haitapunguzwa au kunyimwa kwa ajili ya wazazi kukosa kutoa ilani iliyohitaji ikiwa: (a) Mzazi hajasoma au hawezi kuandika Kiingereza; au (b) Kufuata mahitaji yaliyo hapo juu yanaweza kusababisha madhara makali ya kihisia kwa mtoto.

Habari zaidi kuhusu kuhifadhi utaratibu wako inaweza kupatikana kutoka kwa ifuatayo:

Missouri Department of Elementary and Secondary Education
Compliance Section
Simu: 573-751-0699
Faksi: 573-526-5946
TDD: 1-800-735-2966

Missouri Parents Act (MPACT)
Simu: 816-531-7070
Faksi: 816-531-4777
TDD/Sauti: 1-800-743-7634

Agosti 2009
Idara ya Missouri ya Elimu ya Msingi na ya Upili

Idara ya Elimu ya Msingi na ya Upili katika mipango yake na shughuli zake Haibagui kwa misingi ya umbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia, ulemavu, au umri. Maswali yanayohusiana na mipango ya Idara yanaweza kuelekezwa kwa Jefferson State Office Building, Title IX Coordinator, 5th Floor, 205 Jefferson Street, Jefferson City, MO 65102-0480; nambari ya simu 573-751-9619. Maulizo inayo husiana na programu za Idara na eneo la huduma za Idara, vitendo, na vifaa ambavyo vyafikika hadi na vyatumika na watu walemavu huenda vikaelekezwa kwa Afisi ya Jumba la Taifa la Jefferson, Ridhaa ya Haki za Raia (Kichwa VI/Kichwa IX/504/ADA/ Kanuni ya Umri) Ghorofa ya 5,205 Mtaa wa Jefferson, Mji wa Jefferson, Missouri 65102-0480; nambari ya simu 573-526-4757 au Relay Missouri (800) 735-2966